

MSHINDI WA TUZO YA MTUNZI BORA WA TAMTHILIYA MWAKA 2020

WASOMI WAJINGA



DKT. DYABOLI

WASOMI WAJINGA

tamthiliya, na
Dkt. Dyaboli



KindleDirect Publishing,
North Charleston, SC 29406
www.kdpamazon.com/ebooks

ISBN: 979-8-35480-737-6

Copyright © 2020 Dr. Dyaboli, Mojo
Haki zote zimehifadhiwa.

Hii ni tamthiliya ya kubuni.
Wahusika wote ni watu wa kubuni.
Ushabihiano wowote na tukio, eneo, mtu au kikundi
cha watu halisi walio hai au wafu,
utakuwa ni bahati mbaya.

Wahusika ndani ya tamthiliya

Kizibo. Alikuwa Mkuu wa Kijiji cha Nyinyoro. Kauli-mbiu yake ilikuwa ‘Usipojikaza Unakazwa!’

Madalena. Mwanamke mrembo zaidi kijijini Nyinyoro. Anachukia kuona kivuli chake kikiwa cheusi.

Bila. Mwamini wa Kizibo.

Chegu. Alikuwa mwanajeshi. Sasa ni zombi.

Kichaa. Hata mimi simjui.

Maparara. Kiongozi wa Nyota-ya-Moto. Anaheshimika kwasababu kijiji kizima, ni yeye pekee ndiye alizaliwa akiwa uchi.

Savo. Mmoja wa vijana ambao Kizibo aliwahasudu.

Kigego. Kaka yake Kizibo. Ndiye mtu pekee mwenye meno meupe kijijini Nyinyoro, na ameapa kumshitaki yeyote atakayemuona ana meno meupe kwa ukiukaji wa sheria ya hakimiliki. Ni mbilikimo.

Konde. Alikuwa mfuasi wa Kizibo, sasa ni hasimu.

Makelele. Profesa wa kijiji. Anaziogopa hatua za miguu yake.

Mkyuba. Mwamini wa Kizibo. Ana ugonjwa wa kusahausahau. Hujikumbusha kwa kujipiga kofi kwenye makalio.

Mtoto wa Mganga. Mnyinyoro mwenye fikra-huru. Anamuamini Kichaa.

Mama Wanduta: Mwamini wa Kizibo.

Watu wa Chaki. Wachawi toka Mjini wanaozunguka duniani wakiteka vijiji na kuwaua wanavijiji bila kuwatoa roho. Miili yao ni ya chaki.

Mkunga, Mwalimu, Mtunza-makaburi, Fundi-majeneza, Wanakijiji, Askari, Wanafunzi, Walinzi na Watumishi wa Bucodiavolo, na Wengine

ONESHOKU LA KWANZA

Mandhari ya Kwanza

Sauti toka nyuma ya jukwaa: Dunia ni msumari wa moto, na maisha ni shughuli ya mazishi isiyo na kikomo. Dunia imenipa nini? Mwanzo ni moto, mwisho ni majivu, na katikati ya mwanzo na mwisho ndipo yalipo maumivu yote ya maisha. Watu wanadhani amechukuliwa mtu, lakini si hivyo... kimechukuliwa kijiji! Kwanini msafisha-mazingira alisahau kusafisha macho yangu? Kila kitu ni kiza. Shetani, kudadeki zako! Ee Mungu... Nakuomba uniangazie nuru ya mbalamwezi miguuni panguni ili nione kama kivuli changu bado kipo. *(Jogoo anawika. Muazini anawakumbusha waja umuhimu wa swala. Taratibu pazia linafunguka, mwanga unaanza kulitwaa jukwaa. Linaonekana dampo la kijiji. Pamejaa takataka za kila aina. Upande mmoja wa dampo linaonekana furushi ambalo linatingishika. Linaongezeka urefu. Inaonekana kama miguu ya mtu ikichomoza. Ndio, ni mtu amejifunika kablaniki kadogo kwahiyo ilimlazimu kujikunyata. Anainuka. Ni mwanaume. Ni Kichaa. Anaanza kukagua kama viungo vya mwili wake vyote vipote; anajishika kichwa, maskio, pua na mdomo kisha shingo, anajitazama kiwiliwili na mikono, anachungulia ndani ya suruali yake, anatabasamu. Anajinyoosha na kupiga mwayo. Anajitazama mguuni, ana kidonda kikubwa ambacho kinavuja majimaji.*

Anapiga mwayo tena kisha anabeba furushi lake begani anaondoka akichechemea. Mwanga unafifia. Unaporejea anaonekana mwanaume wa umri wa takribani miaka 35 akikimbia huku akitweta. Anakuja na kuparamia mlango wa nyumba ndogo)

Bila: Madalena! Madalena! Ametoweka! Wamem...
(*anashika kifua na kumeza mate kwa nguvu*)

Madalena: (*kutokea ndani*) Heeeh! Taratibu babu wee, usije ukanivunja mlango! (*anafungua mlango nusu anachungulia akipiga miayo na macho yake yamelegea kwa usingizi*) Nini? Bibi yako ameambukizwa ugonjwa wa Kunengua?

Bila: Wamemtowesha, Madalena!

Madalena: (*anatoka*) Hebu nenda taratibu. Nani ametoweshwa na nani?

Bila: Kizibo! Kizibo Madalena!

Madalena: Kizibo? (*anaganda, kinywa wazi. Sura yake inajaa mikunjo ya huzuni. Anatetemeka. Anafumba macho. Machozi yanambubujika*)

Bila: Madalena, unanisikia? Sema kitu!

Madalena: (*anarejewa na fahamu. Anafumbua macho. Sauti yake sasa ina mikwaruzo anapoongea*) Maskini Kizibo! Unajua nini kuhusu hili, Bila?

Bila: Sijui sana, ila najua vya kutosha. Wapo wanaodai walimuona akinengua, wengine wanasema amezamishwa na sianidi kwenye bahari aliyotaka kutuonesha.

Madalena: Nilijua siku hii ingekuja, ila sikujua... (*ghafla anashika tumbo*) Sssss! Tumbo! Tumbo languu...

Bila: Uko sawa?

Madalena: Tumbo! Kamuite Mkunga! *(Bila anatoka upesi. Anaporejea akiwa na Mkunga, wanamuona Kichaa akiwa amesimama hapo njiani akimtazama Madalena. Mkunga anamuingiza Madalena ndani. Bila anatembeatembea akienda mbele, kisha kurudi alikotoka, halafu anaenda tena. Baada ya kitambo kidogo kinaskika kilio cha mtoto mchanga. Mkunga anatoka akiwa anajifuta uso kwa kutumia sehemu ya nyuma ya viganja vya mikono yake, lakini sura yake imejawa mshangao)*

Bila: Vipi hali yake?

Mkunga: Amejifungua salama.

Bila: Ame... *(anaingia ndani upesi kumuona mtoto. Anatoka akiwa kinywa wazi, anaonekana kuwa na mshangao mkuu)*

Kichaa: Uovu halisi huwa unavutia. Shetani anapokuja kugonga mlango wako, haji kwa sura ya kutisha na mapembe kichwani. Anakuwa na mvuto na anakuahidi haja ya moyo wako, tena kwa sauti tamu kama tarumbeta ya harusi.

Bila: Nini cha kufanya unapoiskia tarumbeta hiyo?

Kichaa: Unaiokoa nafsi yako, au unampa.

Bila: Lakini ukimpa si unalaaniwa?

Kichaa: Lakini hutokuwa peke yako! *(anacheka. Anaiambia hadhira)* Mlio na simulizi za kusimulia simulieni upesi kabla wasikilizaji hawajaondoka!

Bila: Siku zote atapatikana mtu wa kusikiliza.

Kichaa: Labda. Lakini siri ya kuujua ukweli ni kuijua siri.

Bila: Na hiyo siri ni ipi?

Kichaa: Ni siri. Kwanini nikwambie? Siri hazisemwi, zinagunduliwa!

Bila: Toa uchizi wako hapa! Tena potea kabla sijaku...
(*anaokota jiwe na kumrushia. Linampata kwenye paji la uso. Anaokota lingine, Kichaa anakimbia, lakini baada ya hatua chache anaanza kurudi. Jicho lake moja limefunikwa na damu inayochuruzika*)

Kichaa: Hukupaswa kuwa hapa leo. Hili ndilo kaburi lako. Na hutofanyiwa matanga! (*anaondoka. Mbele watu wanaanza kumzonga wakiwa na fimbo na mawe. Sasa wamekuwa kundi kubwa, watoto na watu wazima, wanamcharaza viboko vya mgongo wakiimba:*

“Kindumbwendumbwe...
Chalia!
Kikojozi...
Kakojoa!
Na nguo zake....”

Mbele yao kuna watu wawili wanakuja, mmoja amevalia gwanda za Jeshi la Wanakijiji wa Nyinyoro (JWN) na mwingine amevalia kiraia. Ni Chegu na Savo. Mara tu watu hawa wanapomuona Chegu, wanaacha kumzonga Kichaa, wanatawanyika, mbio)

Chegu: Hivi, nini tofauti kati ya mtoto na mtu mzima ndani ya kijiji hiki?

Savo: Ni idadi ya miaka. Kwanini umeuliza?

Kichaa: (*anasimama kikakamavu mbele ya Chegu, anapiga saluti*) Kamanda! Hakuwezi kuwa na wajenzi bila nyumba ya kujenga, na hakuwezi kuwa na nyumba kama hakuna wajenzi. Kamwe usiandike kwa penseli; labda kama wewe ni mtoto, au uko kitandani na mtu wa jinsia tofauti, au wewe ni mpumbavu! (*anatabasamu*) Lakini usijali Mkuu. Kisasi ni kama ngono; kinapendeza zaidi kikianza taratibu,

kimyakimya, mpaka kinapofikia hatua kikawa hakizuiliki!
(*anapiga tena saluti, anaondoka kwa mwendo wa gwaride*)

Chegu: Kuna kitu ndani ya Kichaa huyu.

Savo: Kweli. Kuna uchizi.

Chegu: Namaanisha kuna kitu spesho ndani yake.

Savo: Hana uspesho wowote. Yuko tofauti tu.

Chegu: Huo utofauti ndio unamfanya awe spesho.

Savo: Kivipi?

Chegu: Fumba macho yako. Unaona nini?

Savo: (*amefumba macho*) Sioni chochote.

Chegu: Basi una uchizi.

Savo: Kivipi?

Chegu: Timamu anapofumba macho huona vitu vingi tofauti. Unaitwa Uwezo wa Kuhuisha Fikra.

Savo: Lakini shuleni tulifundishwa kwamba ukifumba macho huoni chochote!

Chegu: Naamini mlifundishwa pia kwamba kinyume cha nyeusi ni nyeupe.

Savo: Kwani sio?

Savo: Kinyume cha nyeusi ni ‘sio nyeusi’. Inaweza kuwa rangi nyingine yoyote.

Savo: Unamaanisha elimu yetu ni...

Chegu: Nieleze kuhusiana na yule Kichaa.

Savo: Alizaliwa kipofu. Alipofikisha miaka thelathini, mama yake alimtemea mate machoni, akaweza kuona. Lakini msiba mwingine ukafuata kwani miaka mitatu tu baadaye alipatwa na uchizi. Alisema Kizibo alimwonesha njia ya mkato ya kufika baharini, lakini nani amuamini chizi? Huwa

anapotea kwa vipindi virefu; anaporejea husema alikuwa baharini na kwamba ufukwe umemwambia kitu.

Chegu: Utimamu ukizidi unaitwa kichaa — na kichaa kikubwa zaidi ni kuyaona maisha kama yalivyo, sio kama yanavyopaswa kuwa.

Savo: Pia kabla hajawa Kichaa alikuwa anapenda kunusa makwapa ya mchumba wake. Nafikiri alikuwa chizi kabla hata hajawa chizi.

Chegu: Nafikiri alikuwa mjuzi wa mahaba.

Savo: Hapana. Huo ni uchizi!

Chegu: Ulisema tofauti ya mtoto na mtu mzima ni...

Savo: Idadi ya miaka.

Chegu: Okota miguu yako. (*Savo anataka kuinama, anasita, anajicheka*). Pengine Madalena anafahamu chochote kuhusiana na kutoweka kwa Kizibo.

Savo: Lakini Kizibo alikuonesha bahari ilipo, sio?

Chegu: Nitawapeleka. (*wanaondoka. Taa zinazima*)

Mandhari ya Pili

Kiwanja cha michezo cha kijiji. Mawe mengi yamepangwa hapa na yatatumiwa na wanakijiji kama viti kadri watakavyokuwa wakiendelea kuwasili. Tayari wapo wanakijiji kadhaa ingawa ni wachache sana. Yupo Kigego ameketi kwa utulivu. Atakuwa anacheka na kutabasamu muda mwingi, na pale atakapokuwa hacheki, hatabasamu wala haongei, atakuwa anauacha wazi mdomo wake ili kuonesha mwanya na meno yake meupe.

Mwanakijiji-2: Unakubaliana na falsafa ya kwamba mjenzi akijenga nyumba halafu siku chache baadaye nyumba hiyo ikabomoka na kuua mtu ndani yake basi mmiliki wa nyumba anaruhusiwa kumuua mjenzi?

Mtoto wa Mganga: Kama hiyo itamaanisha haki kwa mwenye nyumba na funzo kwa wajenzi wengine.

Mwanakijiji-4: Nafikiri unakanganya haki na kisasi.

Mtoto wa Mganga: Mtu anapoua, akafikishwa mahakamani hakimumu akamhukumu kunyongwa na hukumu ikatekelezwa; hakimumu haitwi muuaji. Niambie; alichokifanya hakimumu ni haki au ni kisasi?

Mwanakijiji-4: Hiyo ni haki.

Mtoto wa Mganga: Kwasababu kitendo kimefanywa na msomi aliyevaa joho na ana leseni ya kufanya mauaji kisheria, sio? Unachora wapi mstari wa kutofautisha haki na kisasi? (kimya)

Savo: Ni mwaka wa nne sasa tangu alipotoweka Kizibo na bado hatujui kwa hakika ni kipi kilimsibu.

Kigego: Zama zimebadilika. Sina hakika kama Wanyinyoro wamekuwa bora, lakini najua wamekuwa tofauti. *(anawasili Makelele akiwa anaendesha tororoo yake ambayo inapiga kelele kali na kufuka moshi. Ni mfupi na mnene sana. Amevalia suruali nyembamba sana ya rangi ya samawati, saspenda, shati la mikono mirefu la hudhurungi pamoja na viatu vya njano. Anaposhuka tu anaangalia saa yake ya mkononi, anasonya)*

Makelele: Kijiji hiki ni mkusanyiko wa akili za sokwe! Kikao tulikubaliana tungeanza saa sita. Sasa inakaribia saa nane na bado wengi hawajafika. *(anajongea. Ghafla anapiga kelele kwa hofu akitazama nyuma yake)*

Mama Wanduta: Hakuna wanaume wengi walio kama alivyokuwa. Alikuwa ni Thomas Sankara mwingine.

Mkyuba: Alikuwa na huu...

Makelele: Mnazungumzia nini?

Mama Wanduta: Kizibo.

Makelele: Cha chupa gani?

Mtoto wa Mganga: Unanikumbusha safari za baharini.

Makelele: *(kwa furaha)* Kwanini?

Mtoto wa Mganga: Kwasababu unatia kichefuchefu.

Mama Wanduta: *(anatabasamu)* Ulitaka kusema nini kaka Mkyuba?

Mkyuba: Mimi? Aam, kuna kitu nilitaka kusema?

Savo: Tulikuwa tumeanza kuuona mnyooko wa mambo, na...

Kigego: Mnyooko? Hilo neno limo kwenye Kamusi?

Mwanakijiji-8: Mzee, maneno mengi ya lugha hayatoki kwenye kamusi – yanatoka kwenye vinywa vya watu!

Mwanakijiji-4: Watu bado hawajashtuka. Siasa ilishavuka hatua ya kuwa taaluma! Kulikuwa na zama ambazo utashi na weledi vilichukuliwa kuwa vigezo vya mtu kuwa kiongozi; siku hizi inatosha kama Mheshimiwa anaweza kukaa kimya halafu akaonesha ubora wa tabasamu lake.

Maparara: Majukumu makuu ya serikali ni kudumisha usalama wa raia dhidi ya hatari toka nje na kudumisha amani na utulivu ndani ya kijiji. Sote tulikuwa moto chini ya Kizibo. Alikuwa na tafsiri yake ya maendeleo – lakini yalikuwa maendeleo.

Konde: Maendeleo? Mtu anapokuwa anahitaji damu hupaswi kumtoa damu tena ili kumwonesha kwamba mishipa yake haijaishiwa kabisa damu. Alikuwa kichaa!

Mtoto wa Mganga: Kwenye vijiji vya Kaanani huwezi kufanya mageuzi makubwa bila kuwa kichaa. Unahitaji kichaa kuchepuka toka kwenye kanuni na mifumo iliyo zoeleka; kichaa kusanifu kesho mpya ya kijiji. Kichaa cha Kizibo kililenga kuleta usawa na kumfundisha kila Mnyinyoro kuvuna mali kihalali.

Mwanakijiji-4: Kwa kuharibu ushindani? Hiyo ilimpora Mnyinyoro hamasa ya kufanya kazi kwa bidii kwani alibaki na matazamio ya kumiliki mali kwa kiwango sawa tu na kila Mnyinyoro mwingine!

Mama Wanduta: Lakini ushindani ulikuwepo dhidi ya vijiji vingine. (*Mkyuba anainuka, anajipiga kofi kwenye makalio akijaribu kukumbuka jambo*)

Konde: Ndiyo, na kama ushindani huo usingeshindwa kwa sababu zingine, basi mafanikio yake yangeuharibu. Nakubali, mafanikio hayo yangeweza kusambaa kwa kasi. Halafu nini? Baada ya kuenea sehemu kubwa ya kijiji, ushindani na vijiji vingine ungekoma na ushindani wa ndani ungeanza. Baadhi ya maeneo ya kijiji yangetajirika kuliko maeneo mengine, na mgawanyo sawa wa huduma za kijamii ungekoma. *(Kichaa anakuja akiwa na tochi inayowaka anawamulika wanakijiji. Anashangaa kuona wanamshangaa)*

Kichaa: Kijiji kinahitaji kuangaziwa. Hapa wanaopaka mafuta tu ndio wanaoonekana. Kwanini?

Makelele: Usawa ni mwanamke ambaye anastahili kubakwa kwenye kitanda cha maiti! Jamani, chura anayevimbishwa alingane na ng'ombe lazima atapasuka, na ng'ombe anayenyimwa kula ili apungue alingane na chura atakufa kwa njaa. Njia pekee ya uhakika ni kumpa kila mtu fursa ya kupata stahiki yake. Niliandika maandiko mengi kumhusu bwana yule na mifumo yake iliyogubikwa upofu, upotofu na utopolo; bahati mbaya zaidi ya asilimia tisini ya Wanyinyoro hawajui kusoma.

Kichaa: Mkuu wa Kijiji hana nguo!

Mwanakijiji-7: Wewe chizi tu.

Kichaa: Lakini msiukatae ukweli kwasababu mimi chizi.

Bila: Hebu tuondolee uchizi wako!

Kichaa: *(anashangaa kumuona Bila)* Wewe? Nilikuona ukiuawa! Huwezi kuwa hai! Mimi sio chizi!

Savo: *(kwa Makelele)* Nilijaribu kuyasoma, nikabaini kwamba usipotumia kauli za matusi unatumia za uchochezi,

na usipotumia zozote kati ya hizo, unaandika uzushi, japo mara nyingi unafanya vyote.

Makelele: Ukosoaji wa kazi za wasomi si kazi yako, bwa'mdogo. Hiyo waachie watu ambao hawakufika chuo kikuu. Wewe jifunze tu ustaarabu utakupendeza.

Mwanakijiji-2: Ustaarabu? Nilikuona juzi unakojolea ukuta wa nyumba ya Mama Wanduta. Unakojolea ukuta, Makelele. Kama mbwa!

Makelele: Ni wale tu waliopata kuishi Mjini ndio wanaweza kuelewa kwamba nilichokifanya ni ustaarabu wa Mjini. Kwenye vyoo vya Mjini mtu anapaswa kukojoa ukutani na mkojo unachuruzika kimyakimya mpaka unafika sehemu husika. Sijui mnanielewa?

Mwanakijiji-3: Mimi nakuelewa.

Makelele: Umewahi kufika Mjini?

Mwanakijiji-3: Hapana.

Makelele: Sasa unaelewa nini?

Mwanakijiji-3: Kwamba Miji inakua kwa kasi kuliko akili za wakazi wa Mijini. (*Mkyuba anajipiga tena kofi kwenye makalio*)

Savo: Maisha yamedinda hadi muda wa kulala hautoshi! Hii imefanya watu wengi wawe na matatizo ya akili. Askari, Manesi na walimu wamezidisha ukali. Watu sasa wanatembea wamekodoa macho kwani hawaoni vizuri kutokana na njaa kali.

Mwanakijiji-3: Wanawake sasa wanaota ndevu na kuwa na sauti nzito kwasababu ya msongo wa mawazo. Na wengi wamekuwa na matumbo makubwa kwasababu ya kula sana viporo!

Mama Wanduta: Wanaume wanazidi kupungua. Imefikia hatua tunaogopa kuzaa watoto wa kiume. Bora wa kike akadange kuliko wa kiume akapandwe!

Mwanakijiji-1: Kigego, hebu tudodosee. Ndani ya familia nduguyo alikuwa mtu wa aina gani? (*Mkyuba anajipiga kofi kali kwenye makalio*)

Kigego: Alikuwa ndugu yangu. Mawazo yangu hayakuwa yake wala yake hayakuwa yangu, lakini alikuwa ndugu yangu. Alipenda ufugaji wa kasuku, lakini aliuchukia ukasuku; na yeyote aliyeonesha ukasuku, bila kujali hadhi yake alimpiga marufuku kuhudhuria vikao vya familia. Na...

Mkyuba: Nimekumbuka! Nilitaka kusema Kizibo alikuwa na huu usemi kwamba ukitembea umbali wa kutosha kuelekea upande wowote unaweza kukiona kisogo chako mwenyewe.

Mwanakijiji-4: Mh! Sio unaweza kukiona kisogo cha mtu aliye mbele yako?

Mkyuba: Ni kisogo chako! Na alisema falsafa hii aliikopa kwa bwana mmoja anaitwaaa... (*anajipiga kofi kwenye makalio*) Mwandishi mmoja wa Mjini jina lake linafanana na parachichi au parachuti.

Kigego: Ni kweli alikuwa anasema unaweza kukiona kisogo chako mwenyewe. Falsafa aliyoikopa kwa mwandishi nguli anaitwa Pratchett.

Savo: Kizibo aliweza kuvunja baadhi ya miamba iliyokimeza kijiji na kwa mara ya kwanza katika historia ya Nyinyoro tulianza kuiona nuru. Sasa miamba hiyo imejengwa tena. (*ghafla kunakuwa na harufu mbaya. Kichaa amejinyea. Wanamkaripia, wanamsukuma, anaanguka, anainuka na kutazama goti lake ambalo limechubuka. Anaingiza mkono wa*

kulia ndani ya suruali yake, anautoa ukiwa na mavi, anaunusa)

Kichaa: Mbona hata haunuki sana kama Bucodiavolo! Au kwakuwa sijanya kwa hisani ya Watu wa Chaki?

Wengine: Kama kila mwanaume angekuwa na mke, mali kiasi na staha, kijiji hiki kingekuwa *Utopia*. Lakini vitu hivyo...

Makelele: Kumbe nanyi mna midomo?

Mkyuba: Muosha-maiti husema kinachoifanya maiti itishe ni kwasababu inakuwa kimya wakati wote. Makelele, sote tunajua ni jinsi gani unapenda kuwa bi-harusi kwenye kila harus na maiti kwenye kila msiba. *(anafika Mwalimu. Makelele anaangalia saa, anasonya akitikisa kichwa. Dakika chache baadaye inasikika kengele ya shule ya sekondari Nyinyoro. Wanaonekana wanafunzi watano wa kike wakija. Wamejipodoa wakapodoka. Wanawapita wanakijiji bila salamu wakisimuliana jinsi mwanafunzi mwenzao alivyomtia ngwara mwalimu darasani baada ya kuambiwa asafishe ubao. Wanacheka sana. Wanaanza kuzungumzia sherehe za maadhimisho ya Mshumaa wa Njano, na sasa wanatumia nguvu kubwa kutikisa makalio yao. Wanakijiji wanamtazama Mwalimu ambaye anawatazama wanafunzi kwa uchu. Anameza mate kwa nguvu)*

Mwalimu: Haturuhusiwi kuwakemea. Wajibu wetu ni kuwafundisha kusoma na kuandika.

Mama Wanduta: Maendeleo. Haya ndio madhara ya VITANDA WAZI.

Mwalimu: *(analazimisha tabasamu)* Ni UTANDAWAZI.

Kichaa: *(anafunua mguu wake. Wanakitazama kidonda chake kwa kinyaa wengine wakitema mate)* Maendeleo ni kidonda. Kinavyozidi kukua ndivyo mguu unavyozidi kuoza. *(Mtoto wa Mganga anaonekana kutafakari sana)*

Mwanakijiji-7: Leo nimebahatika kuunusa Mshumaa wa Njano! Unavutia sana unavyowaka: koroboi si koroboi, karabai si karabai!

Mwanakijiji-4: Kuna daktari husema uvaaji wa chupi ndio umesababisha adha hizi.

Savo: Kivipi?

Mwanakijiji-4: Zamani mabinti walikuwa wanaanza kuvaa chupi wakiwa wakubwa – wakati mwingine katika umri wa kuolewa kabisa, tofauti na siku hizi. Anasema joto la chupi huwanyevua mabinti wadogo na kuwapa mihemko wasiyopaswa kuwa nayo katika umri wao. Hulegeza pia misuli ya via vyao vya uzazi na kuvifanya kuwa vipana. *(wanakijiji wanatazamana kwa soni. Mmoja wa wanafunzi anavua nguo zake na kubaki mtupu)*

Mwanakijiji-1: Wewe binti! Kwanini unavua nguo?

Mwanafunzi: Mambo ya kuvaa nguo yamepitwa na wakati. *(Mwanakijiji-1 anainuka kwa ghadhabu kumfuata, Wengine wanamtahadharisha asitafute matatizo na Mkuu wa Kijiji. Baada ya kuwa wametembea hatua chache wanafunzi hao wanainama kwa pamoja na kuanza kunengua)*

Kigego: Ugonjwa wa Kunengua!! Kimbieni!! *(Wanakijiji wanatoka mbio. Wanafunzi wanaacha kunengua, wanacheke sana. Wanakijiji wanaanza kurejea eneo la mkutano wanapobaini wamechezewa akili)*

Mwanakijiji-2: Nasikia hata kule Chuo Kikuu cha Nyinyoro, mabinti ni wasomi mchana halafu ikifika usiku wanakuwa bidhaa zinazojinadi uchi kwenye madisko.

Makelele: Watoto wa kike hurithi tabia za mama zao – huo ndio msiba wao.

Kichaa: (*anafungua furushi anatoa kitabu; anasoma*) Amini nawaambieni: mwizi, kahaba na fundi-viatu wasingekuwepo kama Mungu asingeuona umuhimu wao. Fundi-cherehani angekuwa wa nini kama Mungu asingempa mwanadamu hisia ya aibu? Wanajeshi wangekuwa wa nini kama wanadamu wasingepewa hamu ya kuuana wao kwa wao? Kati ya taaluma zote maishani, ni mwizi pekee ndiye huwa anakuombea ufanikiwe; ili akuibie. Daktari anakuombea uugue, mwalimu anaomba mwanao awe mjinga, Fundi-majeneza anakuombea ufe, wakili anakuombea upate kesi,... Ha-ha-ha! Hivi kuna wakili mbinguni? Au siku ya mwisho itakuwa ni hukumu bila utetezi? (*anaongea kama wakili*) Mtukufu Mwenyezi Mungu, mteja wangu aliuthamini uhai, ndio maana walimuua. Viongozi wa dini matajiri walimwambia ni sawa kuwa maskini; duniani sio kwetu. Akawaamini. Angeuza nini ikiwa hata cha kuvaa hakuwa nacho? Angefanya kazi gani ikiwa alinyimwa ajira mpaka mazingira ya kujiajiri? Angefanya nini katika jamii ambayo mtu anapoomba chakula au maji hupewa kejeli au masimango? Aliuthamini uhai, Mtukufu; zawadi adhimu toka kwako. Ni kwasababu hiyo wanakijiji walimshambulia kwa mawe kisha wakammwagia petroli na kumchoma moto. Kwasababu aliiba kitumbua kimoja! (*anachora chini alama kubwa ya kujumlisha, anashusha suruali yake mpaka magotini*) Kwa kuhitimisha, ndugu zangu wapendwa, tuko joe njia-panda

kwani hivi punde Mnazarayo mwingine anapelekwa Golgotha.

Bila: Ndio maana ulichizika. Umejawa kufuru!

Mwanakijiji-1: Wasomi, hebu tusaidieni kuuelewa huu ugonjwa wa Kunengua.

Kigego: Ugonjwa huu ulianza kuwala watu nyuma.

Watu kadhaa: Kuwala yuma?

Kigego: Sina maana hiyo. Namaanisha una historia ndefu. *The Dance Plague*, kama walivyouita watu wa Mjini, ulianza kuonekana mnamo karne ya 16 huko Mjini. Kwenye kitongoji kimoja, asubuhi moja majirani walikuta familia ya baba, mama na watoto wao watatu wakishindana kukata mauno. “Familia hii imejawa furaha,” walisema. Lakini ajabu wanafamilia hao waliendelea kunengua kwa masaa mengi na haikuwezekana kuwazuia. Walinengua mpaka wakafa! Siku chache baadaye maambukizi yakaanza kuripotiwa toka maeneo mbalimbali ya mji. Taharuki ikazuka!

Savo: Madaktari walijaribu kila aina ya kinga na tiba. Wakapendekeza kwamba yeyote aliyeambukizwa alitakiwa akatwe kiungo chake cha kwanza kucheza ili asiwaambukize wengine. Na mara zote kiungo cha kwanza kilikuwa ni kiuno.

Konde: Masangoma wakasema anga ilikuwa imezizima; ilitakiwa ipasuliwe kwa kelele. Kengele ziligongwa kwa fujo, bunduki zikafyatuliwa, mbwa walibwekeshwa, watoto wachanga walifinywa, wake na watoto wakacharazwa viboko, na kila mtu alisisitizwa apige kelele kadri alivyoweza.

Kigego: Viongozi wa dini wakasema lilikuwa ni pigo la Mungu. Watu walifurika kwenye nyumba za ibada. Lakini

ilitokea, katikati ya ibada, ghafla kiongozi wa ibada alianza kunengua!

Savo: Daktari mmoja mashuhuri zama hizo aliandika kwamba ugonjwa huu uliambukizwa kwa kutazamana machoni. Andiko lake liliwafanya watu kubaha zaidi. Madaktari walikataa kuwaona wagonjwa, wafanyabiashara walifunga biashara zao, shule zilifungwa na watu wakaanza kuikimbia Miji wakikimbilia vijijini.

Mkyuba: Lakini hata huko likafika. Liliambukiza ng'ombe, mbuzi, nguruwe, kondoo, bata, njiwa na kuku – ambao walikata mauno mpaka wakafa. Liliambukiza mpaka mipapai; ilitikisika hadi ikang'oka ardhini!

Kigego: Watu walikonda kwa hofu. Na katika hatihati ya kunusuru maisha yao, kila mtu alimuogopa kila mtu.

Makelele: Hatimaye serikali ziliweka marufuku kadhaa ili kupunguza maambukizi mapya: marufuku kutazamana machoni, marufuku kusalimiana kwa sauti ya chini na marufuku kujitikisa sehemu ya kiuno.

Mwanakijiji-2: Duh! Kwahiyo watu walikuwa wanatembeaje? *(anafika Askari akiwa na vijana wake wawili. Kichaa anamsogelea anamuuliza ikiwa yeye ni chizi. Askari anamsukuma. Anaangaza macho akimtafuta mtu miongoni mwa wanakijiji hawa ambao sasa wapo wengi sana. Macho yake yanatulia kwa Bila. Anaingiza mkono mfukoni anatoa kikopo cha mafuta)*

Askari: Ni huyo hapo. Mchukueni!

Bila: Nim...nimefanya kosa gani? *(askari mmoja anampiga kofi la uso kisha anamtia vidole viwili puani na kumvuta kwa nguvu)*

Kichaa: (kwa Bila) Nachukia kusema nilikwambia. Lakini nilikwambia.

Bila: Jamani nisameheni! Hak'yamungu sirudii tena!

Askari: (*anamtia ngwara. Anamkanyaga kwenye shingo, anamtemea makohazi mengi usoni kisha anamlenga kwa bunduki*) Usitoe sauti! Na usiwe kimya! 'mamae! Umeuponza!

Maparara: Askari! Hii sio sawa! Unafanya nini?

Askari: (*anatabasamu*) Tunacheza tu.

Maparara: Tunapaswa kufanya mambo yawe bora ndani ya kijiji hiki! Sio hivi!

Askari: (*anamsogelea, anamuwekea mtutu wa bunduki kwenye mdomo*) Ukiona upo mbele ya mtutu, jua nipo nyuma ya kitako! Niambie; unavuja damu ya rangi gani? Unajua ni mbwa wangapi kama wewe nilishawaua na mizoga yao haikuonekana kabisa?

Kichaa: Ahsante Askari! Angalau ulituepushia usumbufu wa kuwazika mbwa hao.

Askari: Ladha ya damu, na ile hisia ya kujing'ata ulimi. (*anampiga kwa kitako cha bunduki kwenye mdomo*) Unazisikiaje? (*Maparara, mikono juu, damu inamvuja mdomoni, anaketi. Askari anarejea kwa Bila, anampanua mdomo, anamgonga kwa kitako cha bunduki, meno manne yanang'oka*)

Bila: Nimetenda kosa gani? Nisameheni sirudii! Mungu nisaidie mimi! Jamani nisaidieni!

Askari: (*kwa Maparara*) Mimi si mpelelezi; ni ncha ya mkuki! (*wanambeba Bila Tanganyika-jeki na kuondoka naye*)

wakiendelea kumpiga mateke na vitako vya bunduki. Kilio chake kinaskika kikififia hatimaye kinatoweka)

Mwanakijiji-5: Hivi wale ni askari wa kweli au ndio WANAJOJULIKANA?

Mkyuba: Kuna askari wa kweli ndani ya kijiji hiki?

Mtoto wa Mganga: Mzee wangu husema hivi karibuni yatazuka machafuko, lakini hayatakuwa makubwa.

Savo: Kwanini?

Mtoto wa Mganga: Mshumaa wa Njano! Mnajua kwanini unazungushwa kijiji kizima? Husema yeyote anayenusa mshumaa huo akili yake hulala.

Mwanakijiji-7: *(kwa mhaho)* Unamaanisha tunarogwa? Si tunaambiwa ainusaye harufu ya mshumaa huo ataishi mara mbili ya umri wa kawaida!

Mtoto wa Mganga: Changanya na zako! *(kimya)* Nilisikia Madalena alijifungua kwa mshtuko siku aliyotoweka Kizibo. Lakini yuwapi mtoto?

Mwanakijiji-1: Mjomba'ke Kizibo aliona Bucodiavolo pangukuwa salama kwa Madalena, lakini si kwa mtoto. Sijui kwanini. *(Mkunga anajawa hofu. Anaondoka)*

Mkyuba: Mara nyingi nimekuwa nikimfananisha na Mnazarayo. Alikuwa radhi kufa hata vifo arobaini.

Mwanakijiji-1: Kwani alikufaje?

Mkyuba: Kizibo?

Mwanakijiji-1: Mnazarayo.

Mkyuba: Zaidi ya robo-tatu ya dunia inalijua hilo. Alikufa kwa kuhangikwa msalabani!

Kichaa: Ha-ha-ha-ha!

Mkyuba: Unajichekesha nini? Unataka tiba ya Chekelea?

Kichaa: Waogope wanaocheke. Hujui ikiwa wanacheke na wewe au wanakucheke. Nakucheke wewe na zaidi ya robo-tatu ya dunia.

Mkyuba: Mpumbavu mmoja wewe! Haya, alikufaje?

Kichaa: Mkuki wa ubavu! Mpumbavu wa pili wewe!

Mwanakijiji-2: Wengi tumeshajaribu mara nyingi kuondoka katika kijiji hiki lakini kila tuendako, tunajikuta tunatokea tulipoanzia! Makelele, wewe ni profesa; tusaide jinsi ya kufika baharini!

Makelele: Kizibo aliamini alikuwa anajua kila kitu, na mtu anapokuwa na mtazamo huo, hawezi kukosa mazuzu wa kumuunga mkono. *Aut neca aut necare!*

Mwanakijiji-6: Labda tumuombe Kichaa atusaidie.

Makelele: Tumuombe Kichaa? Bila shaka wewe ni kichaa pia.

Mama Wanduta: Dunia inahitaji watu wangapi wanaowakimbia wengine kwasababu tu wao wenyewe hawajioni? Maisha yenyewe ni wazimu, nani anajua kichaa kimo ndani ya nani?

Makelele: Sina muda wa kuzozana na mwanamke.

Mama Wanduta: Nguvu haitokani na kile ulichonacho katikati ya mapaja. Mwanamke ana nguvu kuliko mwanaume katika mambo mengi.

Makelele: Mwanamke ni mkusanyiko tu wa vitu kama nywele ndefu, matiti, nyonga pana, ku...

Savo: *(anamfokea)* Mama'ako ni mwanaume?

Makelele: ...kucha ndefu, *(anasita)* Halafu na we' dogo usinifokee!

Savo: Dogo baba'ako! (*Makelele anainuka kwa jazba, lakini wakati huohuo anaonekana Askari akija tena, sasa ameambatana na vijana wake takribani ishirini hivi na wamebeba dumu la mafuta. Wanakijiji wanamtazama Kichaa*)

Kichaa: Palipo na askari wengi hapana usalama!
(*wanatawanyika wakikimbia. Pazia linashuka*)

Mandhari ya Tatu

Chumba kidogo cha hadhi ya kati chenye kitanda, kiti kimoja na meza. Mezani pana ramani ya kijiji cha Nyinyoro na karatasi moja nyeupe iliyoandikwa ‘MVUA ITAKAPONYESHA NDIYO MTAJUA PANAPOVUJA’.
Vilevile pana banda nadhifu la ndege ambalo ndani yake mna kasuku watatu walionona. Kizibo amekaa kitandani, Madalena amekaa kwenye kiti mbele yake. Ni majira ya jioni.

Kizibo: Ndani ya kijiji hiki watoto wanaogopa giza, wakubwa wanaogopa mwanga. Waliokula chumvi nyingi matendo yao hayana ladha.

Madalena: Unapaswa kujifanya unaamini kile ambacho kila mtu anakiamini – au angalau uwaache wengine waamini kile wanachoamini. Hiyo ni salama!

Kizibo: Ni rahisi kukwepa wajibu kuliko kuwajibika.

Madalena: Simaanishi hivyo.

Kizibo: Kijiji hiki kina bahari kubwa; lakini asilimia 97 ya wanakijiji hawajawahi kuiona. Na wanaojua ilipo hawataki wengine wajue. Wengi hata ukiwambia kijiji hiki kina bahari wanakuona kichaa. Uovu umezama ardhini kiasi kwamba hauwezi kuondoshwa kwa ibada au hata kwa mvua ya jiki. Uonevu, rushwa na ubadhirifu vimeshamiri. Kijana kupata ajira ni mpaka awe na mtu wa kumshika mkono au awe chawa; kama ni binti basi ahonge ngono. Kwenye soko la ajira mabinti wenye makalio makubwa wanathaminiwa kuliko

wenye elimu kubwa kiasi kwamba sasa mabinti wanatafuta makalio kuliko elimu! Unafikiri siyajui haya? Nitazame Madalena! Nimedhamiria kukivunjavunja kijiji hiki na kukijenga upya ndani ya miaka michache tu!

Madalena: Sote twajua kuwa ndani ya kijiji hiki ukiwa masikini wewe ni mpumbavu. Na hakuna anayemskiliza mpumbavu. Unaweza kupata vitu vingi ukiwa na pesa!

Kizibo: Ni kweli; unaweza kupata hadi dhambi! Mtazame Konde. Watu wanahoji kwanini nimempiga marufuku kuhudhuria vikao vya familia. Lakini nakwambia; usalama wa kijiji unatingishwa toka ndani na nje. Kutoka ndani, na wanasiasa makasuku kama Konde na Makelele ambao wako radhi kuutoa kafara usalama wa kijiji kwa maslahi yao binafsi. Konde anapenda kucheza kwenye mvua kama mwanamke halafu hataki kuolewa, na Makelele ni mwanamke wa leo wa Nyinyoro anayeota kuwa mwanaume kesho! Kutoka nje usalama wa kijiji unatingishwa na Watu wa Chaki na huu wimbo wao wa Makanjanja. Chukulia huu ugonjwa wa Kunengua kwamfano; hivi hata unauelewa? Imefikia hatua hata wanandoa wanapokuwa faragha, mwanamke akijaribu tu kucheza kiuno, mwanaume anatoka mbio akihofia mkewe amepatwa na ugonjwa wa Kunengua! Watu wanawezaje kuwa na furaha ikiwa wanaishi kwa hofu wakati wote? Ndio sababu nimeamua niwazibe macho na masikio Wanyinyoro ili wasione wala kusikia chochote cha kuwatisha. *(Kimya. Anaichukua karatasi iliyopo mezani, anayatazama sana maneno yake)*

Madalena: Hiyo falsafa ya mvua. Unaihusudu sana.

Kizibo: Tangu nikiwa kiranja wa mazingira shuleni wenzangu walikuwa wakiniambia napoteza muda kuwafundisha kenge kupaa angani. Lakini najua siku moja watanikumbuka.

Madalena: Mkakati wako ni upi?

Kizibo: Kuwapanua Wanyinyoro wote! Na tayari nimeanza na vijana kwa kuwaingizia...

Madalena: Kuwapanua?

Kizibo: Kimawazo. Kwa kuwaingizia darubini kwenye mitaa na vitongoji vyao ili waweze kuiona bahari. Watu hawawezi kwenda baharini mpaka wawe na uhakika bahari ipo. Wakisita nitawalazimisha! Kubanda aliwahi kusisitiza kwamba kinachomzamisha mtu sio kudondoka mtoni bali ni kushindwa kupiga mbizi.

Madalena: Kubanda? Sikuwahi kumsikia mtu huyo.

Kizibo: Alikuwa anazungumziwa sana kwenye siku zake; hasa na yeye mwenyewe.

Madalena: Tu watumwa wa asili zetu, Kizibo. Huwezi kujizidi mbio! Unachofanya ni...

Kizibo: Vita. Dhidi ya kila kilicho kwenye njia ya kutufikisha tunakopaswa kufika. Mbwa 1000 wakiongozwa na simba mmoja, hao mbwa wote wanakuwa simba; na simba 1000 wakiongozwa na mbwa mmoja, wote wanakuwa mbwa!

Madalena: Ana heri mtu mpole kuliko mtu wa vita; mtu aidhibitiye hasira yake kuliko yule autekaye mji.

Kizibo: Nimekuwa nikiona mambo Madalena, mambo ambayo mtu wa kawaida hapaswi kuyaona.

Madalena: Mambo ya aina gani?

Kizibo: Maono ya mambo yajayo. Nitasalitiwa na watu ninaowaamini sana, lakini nitakumbukwa kwa mazuri nitakapokuwa nimeondoka.

Madalena: (*anatafakari*) Mimi naogopa!

Kizibo: Siku zote fanya unachoogopa kukifanya.

Madalena: Kwanini?

Kizibo: Woga ni kizuizi cha Shetani kati ya mwanadamu na mambo mazuri.

Madalena: Lakini ni hatari!

Kizibo: Ukitaka kilicho bora, hakuna njia rahisi. Inahitaji sadaka! Kuwa na imani; Mungu yu upande wetu.

Madalena: Wanasema ni Mungu mwenye nguvu. Lakini wengi wa watu wake wanafeli vita vya maisha!

Kizibo: Huko ni kutishwa na hisia zako mwenyewe. Isitoshe, hata wakiniua sitabaki kuwa mfu – nitarudi! Inaweza kuchukua miaka au hata miongo kadhaa, lakini nitarudi! Mahali fulani, mbegu itachipua, itastawi, na siku moja Kizibo atainuka tena!

Madalena: (*anaiambia hadhira*) Baadhi ya watu hawakuumbwa kwaajili ya maisha ya vijijini.

Kizibo: (*anapoona Madalena amepoa ghafla*) Tafadhali usianze hiyo.

Madalena: Nikiomba tuzungumzie mada tofauti, utapenda tuzungumze kuhusu nini?

Kizibo: Kuhusu wewe.

Madalena: Huwa inakufurahisha kuzungumza kuhusu mimi?

Kizibo: Huwa inakuumiza?

Madalena: Wakati mwingine

Kizibo: Oh! (*kimya*)

Madalena: Mbona umekuwa kimya ghafla?

Kizibo: Umenizuia kuzungumza kuhusu wewe ilhali wewe ni mada ninayoihusudu.

Madalena: Basi tuzungumze kuhusu mapenzi.

Kizibo: Neno Mapenzi lina tafsiri kumi na sita. Unalenga ipi?

Madalena: (*baada ya kusita kidogo*) Mie napenda ufanye mapenzi, sio vita.

Kizibo: Hata mapenzi ni vita. Wale wanaozijua mbinu za mapenzi wanakuwa wafalme au malkia, wasiozijua wanakuwa wapambanaji au watumwa.

Madalena: Ha-ha-ha! Hivi, kama nyoka angemshawishi Adam kula tunda badala ya kumshawishi Hawa kama alivyofanya, unaamini asingefanikiwa?

Kizibo: Kama ningekuwepo, ningehakikisha hafanikiwi.

Madalena: U mtu mwema Kizibo. Lakini unafikiria sana. Hiyo inakutafuna!

Kizibo: Mwanaume anapaswa kukipenda kijiji chake kwa akili yake yote, ampende kiongozi wake kwa nafsi yake yote, ampende mkewe kwa moyo wake wote, na ampende mungu wake kwa akili, nafsi na moyo wake wote.

Madalena: Kupenda ni kubaya. Kutopenda ni kubaya zaidi.

Kizibo: Kati ya maovu mawili, mtu anapaswa kuchagua ovu dogo.

Madalena: Lakini kwanini mimi?

Kizibo: Wewe ni muujiza! Watoto wangapi wanazaliwa wakiwa wajawazito? Tofauti kati yako na malaika ni mabawa tu. Na bado siku zote umejionesha kuwa mnyenyekevu,

mwenye hekima, na u mrembo kiasi kwamba kila akutazamaye hufarijika. Hata ukigeuka mbwa, nitakuhudumia vizuri kama daktari wa wanyama!

Madalena: *(kwa hisia kali)* Nakuahidi Kizibo; hata mbwa-mwitu wajapotufikia na kuvunja mlango wetu nitashikamana nawe mpaka kwenye bonde la uvuli wa mauti. *(kimya. Anajikunyata)* Leo kuna baridi!

Kizibo: Zipo njia nyingi za kusema nakupenda ndani ya dunia hii ya baridi. Njoo kipenzi, nikuoneshe jinsi ya kulikumbata jua. *(Madalena anambusu kwenye shavu. Kutoka nje Chegu anagonga mlango kwa fujo akipayuka 'Gethsemane!' Madalena anashtuka toka usingizini. Alikuwa anaota. Mandhari inabadilika. Yumo chumbani. Kama katika ndoto, chumba hiki pia ni kidogo chenye kitanda, kiti kimoja na meza. Lakini juu ya meza hii pana chupa kadhaa zilizojaa damu, simu ya mezani pamoja na mkoba. Hiki ni chumba cha hoteli, ni Mjini, na ni majira ya jioni. Anapoamka tu anamuona Mtu wa Chaki amekaa kwenye kiti akichakura magazeti ya leo)*

Mtu wa Chaki: Umekuwa ukiota tena. Nimekuona ukiweweseka.

Madalena: Bado upo hapa. Kwahiyo nina hakika sikuwa nanengua usingizini.

Mtu wa Chaki: Ni ndoto ileile ya siku zote?

Madalena: *(anafikicha macho na kuondoa tongotongo kwa kutumia shuka la hoteli)* Ugeniamsha. *(anakwenda kufungua mkoba wake. Anatoa viatu vya Kizibo na kuvivaa lakini kutembea anashindwa.)*

Mtu wa Chaki: Utawala wa Kizibo haukuwa jambo la kuonewa ufahari. Sielewi kwanini unatamani ungeweza kuvitembelea viatu vyake.

Madalena: Wanawake wote huwa wanajua mwanaume anayezungumziwa sana ni lazima huwa ana kitu fulani cha kuvutia ndani yake. (*kwa aibu*) Alikuwa mtu mwenye jina. Na mtu anapaswa kujitoa sadaka ili kuweza kuacha jina kama aliloliacha yeye.

Mtu wa Chaki: Sio kosa kusema mtu asiyekuwepo hayupo!

Madalena: Ni kosa kumshambulia asiyeweza kujitetea.

Mtu wa Chaki: Watu huwa hawakosi visingizio vya kuwatetea wale waliowahusudu, ambao walishindwa baada ya kuwa wamebwata sana. Hivi unajua kwamba kubakwa juu ya kitanda cha mfalme kuna heshima yake?

Madalena: Mimi ni mwanamke, sio mwanaizaya.

Mtu wa Chaki: (*anamkazia macho, anashusha pumzi ndefu*) Umeleta damu kiasi gani awamu hii?

Madalena: Ya kutosha.

Mtu wa Chaki: (*anasogea mezani na kuibeba chupa kubwa iliyojaa damu. Imeandikwa NYINYORO*) Bado asilimia themanini ya deni lako.

Madalena: Tafadhali ibebe vizuri chupa hiyo. Ina maisha ya Wanyinyoro wengi.

Mtu wa Chaki: Ushauri mdogo nikupe: Wakikupenda utawaongoza; wakikuogopa utawatawala. Ni salama zaidi wakikuogopa! Epuka kuomba radhi unapokosea, na pia epuka kukiri umekosea. Ukikiri hata mara moja kwamba umekosea, wapinzani wako watafanya ionekane kama kila unachokifanya

ni makosa. Usiwape silaha hiyo! Ukitaka ufike kwa wakati huko uendako, beba vile tu utakavyovihitaji kwenye safari yako. Na ukitaka wakuogope, kamwe usimuue mtu bila kukusudia! Historia imelithibitisha hili.

Madalena: Nitaukumbuka ushauri wako. (*pazia linafunga*)

ONESHOK LA PILI

Mandhari ya Kwanza

Bucodiavolo. Ni jengo la kifahari lenye ghorofa tatu. Hii ndio ikulu, anapoishi Mkuu wa Kijiji. Kutoka ndani inaskika sauti ya mwanamke akipambana na mtu. Pazia linapanda. Ni asubuhi. Madalena yupo kwenye eneo la wazi, amevalia kaptula na kizibao cha JWN na ana upanga anafanya mazoezi. Kando yake amesimama Mlinzi-1, na mita takribani ishirini upande wa kusini kuna farasi watano. Inaskika pia redio na sasa unapigwa Wimbo Mtakatifu wa Makanjanja:

“Mtoto akizaliwa na fuvu la Kichaa, mbamize ukutani.

Wengine waue tumboni, zaa wachache kisomi.

Vizibo vyote toa – walevi walewe kwa amani.

Otesha uoto wa kisasa – ua wa asili.

Tiba za jadi ni ushamba – usasa ni hospitali.

Ukipewa mkopo – pokea – usilete ukaidi.

Mtu akiishi miaka 60 – muue asiishi zaidi.

Mtu wa Chaki akinya mchambe; kinyaa ni ugaidi.

Mnepewa supu ya mguu wa kuku, katiანი vidole.

Mnapendwa, mnapewa mikopo ili mkalie na ndizi.

HEBU ACHENI UBAZAZI!

SHABANI AKIMUOA JUMA, KWANI TATIZO NINI?

MARIA AKIOLEWA NA JENI, INAKUUMA NINI?

.....”

Madalena: *(anakitazama kivuli chake kwa kinyaa. Kwa Mlinzi-1) Hebu zima hiyo redio!*

Mlinzi-3: *(anaingia) Mama, kuna mgeni wako. Ni... Ni... Ni Maparara.*

Madalena: Kusitasita ni ishara ya udhaifu wa mwili kwa mzee, na udhaifu wa akili kwa kijana. Makinika! Mruhusu *(anaendelea na mazoezi. Maparara anapoingia tu, Madalena anachukua upanga mwingine anamrushia. Wanaanza kukabiliana)*

Maparara: Vita vya zama hizi havipiganwi kwa upanga – vinapiganwa kwa ubongo!

Madalena: Kazi ya upanga ni kuutia makali ubongo. Mwili dhaifu hauwezi kubeba ubongo shupavu. *(anakitazama tena kivuli chake. Ghafla anatoa ukelele wa maumivu. Upanga wa Maparara umemla kwenye bega, damu inachuruzika)*

Maparara: Oh! Sssamahani dada ya... *(Madalena anamvamia kwa jazba. Anajitetea akiwa anarudi nyuma)* Madalena! Madalena acha! Madalena acha tafadhali! *(Mlinzi-1 anawahi na kumshika Maparara kwa nyuma akimbana barabara ili atiwe upanga. Madalena analeta upanga kwa nguvu, Maparara anapiga kelele)* MADALENA ACHAA!!

Madalena: *(anazinduka) Ah, kaka Maparara! (anautazama upanga wake mkononi, anauachia, anakwenda kuketi kwenye benchi. Maparara bado anatetemeka na nzi wanaanza kumzonga. Anamtazama Mlinzi-1 kwa macho makali, mlinzi anatabasamu kifala)*

Maparara: Uko sawa dada? Samahani, sikukusu...

Madalena: Ni kajeraha kadogo tu. Kuwa na amani. Nimebeti halafu kuna katimu kamoja kamenichania mkeka,

ndio kamenitia hasira. (*anacheka, sasa akiwa amefika Mtumishi analihudumia jeraha lake*)

Maparara: Una akili kama yangu.

Madalena: Hapana. Una akili kama yangu.

Maparara: (*wakati Mtumishi anaondoka*) Yule Mtumishi aliyeletwa na Kizibo yuko likizo?

Madalena: Waliniambia alikuwa kichwamaji, nikakubali aendelee kunifanyia kazi. Lakini ajabu, kila nilipojaribu kuwachekesha, wengine wote hapa Bucodiavolo walikuwa wanacheka, isipokuwa yeye tu. Halafu kama hiyo ilikuwa haitoshi, akaanza kulalamikalalamika. Nikabaini hakuwa kichwamaji, ikabidi nimtimue. Kazi ya mfanyakazi ni kufanya kazi, sio kulalamika.

Maparara: Ni rahisi kuwachekesha wapumbavu; ndio maana siku hizi watu wengi wanajiita wachekekehaji. (*anasita kidogo*) Halafu, mara nyingi ninaposoma maandishi yaliyoandikwa mbele ya jengo hili huwa napata mtanziko.

Madalena: BUCODIAVOLO?

Maparara: Yale madogo ya chini yake yanayosomeka ‘Nyinyoro mlinde mungu’. Sio kwamba yalipaswa kuwa ‘Mungu ilinde Nyinyoro’?

Madalena: Mchoraji aliyepewa kazi hiyo alikuwa anatumia mkono wa kushoto; ndio sababu akaigeuza sentensi. Kumleta mwingine yatakuwa ni matumizi mabaya ya kodi za wanakijiji. (*kimya*) Kwahiyo, niambie; maisha yanakutendea uungwana?

Maparara: Siwezi kulalamika dada. Niliposikia tu umerejea toka Mjini nikasema nijitahidi nije nikuone kabla hujaondoka tena, maana nyinyi wakubwa ratiba zenu

zimebanana. Hivi kuna tofauti gani kati ya maisha ya Mjini na ya kijijini?

Madalena: Ni kwamba tu mtu anapokuwa Mjini anaburudika; anapokuwa kijijini anawaburudisha wengine. Na kuongea Kinyinyoro wakati wote kunachosha, ndio sababu wakati mwingine tunaamua kutoka kidogo twende mahali ambako watu hawazungumzi Kinyinyoro.

Maparara: Nakuelewa. Naona mambo sio mabaya; unazidi kunenepa.

Madalena: Aaah, kaka! Umeanza. (*anasimama kijivuni, anajizungusha*) Unaweza kunijibu kiukweli? Ukweli kabisa?

Maparara: Bila shaka.

Madalena: Hivi mimi ni mrembo?

Maparara: Unatosha kwa malengo yote ya kawaida. Lakini..., umevaa?

Madalena: (*baada ya kujitazama*) Unanitusi?

Maparara: Hapana. Kichaa husema mara kwa mara kwamba Mkuu wa Kijiji hana nguo, kwahiyo nikataka...

Madalena: Aagh, ana wazimu yule.

Maparara: (*anainong'oneza hadhira*) Ndugu zangu, ukweli mbaya sio kitu ambacho mwanaume anapaswa kumwambia mwanamke! (*kwa Madalena*) Hata hivyo nina hofu juu yako. Hali yako sasa ni kama mtu anayekufa kutokana na kuwa na afya kupindukia.

Madalena: Kaka, una moyo wa kiungwana kwenye mchezo wa vurugu. Kuhurumia bila uwezo wa kusaidia kunaumiza kuliko kuomba ukakataliwa! (*anatabasamu*) Haya, kuna nini?

Maparara: Watu wanaongea.

Madalena: Kuhusu nini?

Maparara: Hali ya maisha.

Madalena: Wanyinyoro! Hata uweje, hawatokosa mawe ya kukurushia. Labda kwasababu kijiji hiki kina milima mingi yenye mawe lukuki. Kwanza... mimi ni mwanamke; kwanini hamnitii?

Maparara: Aam, unataka kuti...

Madalena: Kana kwamba hamkuzaliwa na wanawake! Hamuwezi hata kunitii kama mama au dada yenu?

Maparara: Ni rahisi mtu kuwa mwema anapokuwa na furaha, kama tu ambavyo mwanaume huweza kumhurumia mkewe kwa kazi ya upishi pindi chakula kinapokuwa kitamu. Biashara pekee inayolipa kwa sasa ni ya vichekesho. Hii inamaanisha watu hawana furaha!

Madalena: Unawezaje kuwa na furaha ikiwa huyapendi maisha yako? Unapaswa kuyapenda maisha ili uwe na maisha!

Maparara: Na unapaswa kuwa na maisha ili uyapende maisha. Wape nyama wanyamaze!

Madalena: Nimechoshwa na huu werevu! Siku hizi kila mtu anajua kila kitu. Nakuapia; huwa simuumizi mtu bila yeye mwenyewe kunisaidia.

Maparara: Shida ni utiifu wako kwa Watu wa Chaki.

Madalena: Kaka Maparara, wanawake wote ni waongo. Wachawi hawa wanafikiri wananitumia, lakini kiukweli, ninawaongopea. Dira yangu ni kuwashinda kwenye mchezo wao wenyewe.

Maparara: Unakwenda kasi sana. Kukimbia duniani kasi kiasi hicho kama wembe ulio uchi, una hatari kubwa ya

kukikata kijiji. Usisahau; anayetaka kula na Shetani anapaswa kuwa na kijiko kirefu!

Madalena: Kaka, kuishi ni kuhakikisha hauishi; na hatua ya kwanza ni kujua tofauti kati ya unachotaka na unachohitaji. Safari yangu ya kisiasa imenifunza kwamba wakati mwingine njia pekee ya kufika unakotaka ni kuwasaidia wengine wafike kwanza wanakotaka kufika.

Maparara: Siamini unaamini hivyo.

Madalena: Siamini huamini naamini hivyo. (*kimya*)

Maparara: Vipi maendeleo ya Chegu?

Madalena: Kichwa chake sio chake, lakini ni yeye.

Mtumishi: (*anafika*) Mama, Chegu kaamka.

Madalena: Hasemwi! Ana maisha marefu. Twende tukamuone.

Maparara: Vipi yule askari anayelalamikiwa kwa rushwa na kuamuru kila kaya impe binti wa kulala naye?

Madalena: Tulijumlisha, tukatoa, tukazidisha na kugawanya, tukabaini tatizo. Tatizo ni kwamba kujumlisha, kutoa, kuzidisha na kugawanya hakukuwa na tatizo. (*anawaza*) Tumemhamisha kituo cha kazi.

Maparara: Na nimesikia kuhusu muswada wa sheria ya wanakijiji wote kutakiwa kutembea na vichwa vyao ndani ya mifuko. Kuna shida gani vichwa vikiendelea kubaki juu ya shingo?

Madalena: Watu hawajui jinsi ya kuvibeba vichwa vyao kwa manufaa ya kijiji.

Maparara: Nafikiri...

Madalena: Nani kakuruhusu kufikiri?

Maparara: Lakini dunia yote inategemea watu wanaoweza kufikiri kikubwa!

Madalena: Watawala! Wajibu wa wanakijiji ni kufuata wanachoambiwa. Wanapaswa wafanye kile kinachoipendeza serikali, sio kinachowapendeza wao. Kwahiyo wanatakiwa kuzuiliwa kabla hawajaanza kufikiri. Ndiyo sababu nimeamua niiuze anga ya Nyinyoro, niwauzie Watu wa Chaki. Hii itasaidia Wanyinyoro wasipate nafasi ya kufikiri kwani watakuwa wanatazama angani muda wote. *(wanaingia kwenye chumba kimojawapo. Ni kikubwa lakini kina vitu vichache tu: kitanda kidogo na meza ambayo juu yake pana daftari na penseli. Vilevile kuna saa ukutani na banda chakavu la ndege ambalo ndani yake mna kasuku mmoja aliyekondeana. Chegu amelala kitandani akitazama dari)*

Maparara: Chegu, habari yako kaka? *(kimya)*

Madalena: Kaka Chegu, ni Maparara. Anataka ajue unavyojiskia ili ujue anavyojiskia kuhusu unavyojiskia. *(kimya. Madalena anakwenda mlangoni na kutoa gwanda za jeshi za Chegu, anamwonesha. Chegu anafurahi, anatega sikio kana kwamba anasikiliza jambo darini. Anachukua penseli na daftari. Anakunja sura)* Unafanya nini kaka Chegu?

Chegu: *(anaandika)* Nakisikiliza kijiji.

Madalena: Unasikia nini?

Chegu: *(anaandika)* Kila kitu.

Madalena: Unaweza kutwambia tafadhali?

Chegu: *(anaandika)* Sina ulimi.

Maparara: Kwanini umemuonesha hizo gwanda?

Madalena: Ukumbusho wa siku zake za utukufu.

Maparara: *(kwa huzuni)* Alikuwa mwanajeshi mahiri. Kila mtu alimuogopa. Lakini siku hizo zilikwishapita. Anakuwa hivi wakati wote?

Madalena: Siku aliyotoweka Kizibo, unajua niliona nini?

Maparara: *(kwa shauku)* Uliona nini?

Madalena: Sikuona chochote. Nilihisi kama Kijiji kilikuwa kimekufa nimeachwa nyikani. *(analia kwa kwikwi)* Natamani Kizibo angekuwepo – walalu hata katika hali kama ya Chegu. Namkumbuka sana jamani! Siko tayari kumpoteza mwingine yeyote kati yenu! *(anazidisha kilio akifuta machozi kwa kisigino cha kiganja cha mkono wake)*

Maparara: Pole dada'ngu. Siwezi sema najua unavyojisikia, lakini... *(anaingia Mtumishi. Maparara anasogea lilipo banda la kasuku. Anaingiza kidole bandani lakini kwa hasira kasuku anamdonoa. Kando ya banda anaona nyaraka zinazoelezea gharama za matibabu ya kasuku huyo zimeambatanishwa na cheki ya milioni 921 imesainiwa na Madalena)*

Mtumishi: Samahani mama, nimekosea dawa Chegu nimempa vile vidonge vya mbwa.

Madalena: Hakuna shida. Hatobweka sana.

Mtumishi: Halafu daktari hajafika leo. Na muda wa sindano kwa mgonjwa unakaribia kupita.

Madalena: *(anaangalia saa ukutani)* Chukua sindano umdunge kabla hatujachelewa zaidi.

Mtumishi: Mama! Mimi?

Madalena: Oh, nilisahau unaogopa kuona kitu kikitoboa mwili. Muite mlinzi mmoja aje amdunge. *(Mtumishi anatoka)*

Maparara: Kwani huyu daktari mwenyewe ni yupi?

Madalena: Unamkumbuka yule kijana mrefu mtoto wa Mama Tangode yule dada wa shoga'ke mama?

Maparara: Ni yule aliyefukuzwa chuo kikuu mwaka juzi baada ya kusemekana alimlevya mkufunzi wa kiume kwa *Burundanga* kisha akamf..., akamuingilia kinyume na maumbile?

Madalena: Kumbe hujazeeka bado kaka yangu.

Maparara: Hivi kesi yake iliishaje? Na... nakumbuka wakati anafukuzwa alikuwa mwaka wa kwanza chuoni hapo; kwani alimaliza chuo?

Madalena: Unajua, mtu anaweza kuona vitu vingi anapokuwa na njaa. Waliodai wangetoa ushahidi dhidi yake mahakamani niliwambia waje hapa wanieleze walichokuwa wamekiona; hakuna aliyekuja. Na hata mahakamani hakuonekana hata mmoja wao. Ha-ha-haa. Ni makosa kufikiri kila aliye na milango mitano ya fahamu ana fahamu! Na... Chuo hakumaliza. Lakini kwakuwa cheti chake cha ubatizo kilisainiwa na padri aliyenibatiza mimi, nikaona kwanini nisimpe nafasi awe anawatibu kaka Chegu na wengine!

Maparara: Halafu nimekumbuka jambo... Hivi yule kijana aliyevunjwa kidole akakikimbia kijiji bado hajarejea Nyinyoro?

Madalena: Aliumia sana. Fikiria... bila mafuta! (*anashusha pumzi ndefu*) Nimemwambia mara kadhaa arudi nyumbani kwani sasa ni ruksa wakubwa kutembea na mafuta, sijui bado anasita nini! (*anatabasamu*)

Maparara: Mafuta. Sawasawa. (*anamtazama sana*)

Madalena: Jicho la wema?

Maparara: Nawaza tu: dakika mbili zilizopita macho yako yalikuwa yamejawa machozi – sasa uso wako umesawijika na u mwenye furaha. Unabadilika haraka!

Madalena: Siasa ni kama kipindi cha luninga; ukishindwa kuteka hisia za hadhira kwa haraka, wanabadili chaneli.

Maparara: Kweli. Nakumbuka miaka sita nyuma hukutaka kuishi ndani ya nyumba hii; leo hutaki kutoka.

Madalena: Huwa unasoma Biblia kaka Maparara?

Maparara: Sio mara kwa mara.

Madalena: Basi leo kasome Kitabu cha Kutoka. Kitakusaidia kuelewa kwamba kuingia huwa ni rahisi lakini kutoka ni mtihani. (*anaingia Mlinzi-4*)

Mlinzi-4: Naam mama.

Madalena: Angalia kwenye droo ya meza kuna chupa ya dawa, chukua sindano umdunge Chegú.

Mlinzi-4: (*anatoa chupa iliyoandikwa SCOPOLAMINE*) Mama, sindano nachukua bomba dogo au kubwa?

Madalena: Sijui uchukue dogo, sijui kubwa. Dogo litatosha. Au chukua kubwa. Ah, au chukua tu lolote.

Mlinzi-4: Dawa naweka kipimo gani?

Madalena: (*anamtazama Maparara, anabetua mabega kuashiria hajui pia*) Kadiria tu utakayoona inatosha.

Mlinzi-4: Samahani Mama; namchoma sehemu gani?

Madalena: Huoni kama nina mazungumzo? Acha usumbufu! Muhimu si ni dawa iingie mwilini? Choma sehemu yoyote!

Mlinzi-4: Sawa Mama. (*anajisemea*) Kwenye kichwa ndio dawa itafanya kazi haraka. (*anamdunga kwenye utosi*)

Madalena: (*analetewa simu na Mtumishi, inaita, anaiweka sikioni*) Mnh? Bado anafuatilia kutaka kujua zaidi? (*anajibiwa. Anaonekana kuwaza*) Hatakiwi kuona zaidi. Ongea na Skopioni. (*anamrudishia simu Mtumishi. Anamtazama Maparara*) Bahati nzuri kila mtu ambaye yuko sahihi huwa anakubaliana nami. Niko sahihi kaka?

Maparara: Kamwe hukosei!

Madalena: Nilikuwa nimefikia wapi? ...oh, hata wazazi wanaumia sana kuona mabinti zao wakikatisha masomo kwasababu ya kupata ujauzito shuleni. Kwanini kuwa wanawake ndio iwe dhambi ya mabinti zetu? Kwanini? Hatuwezi kuendelea kulifumbia macho suala hili. Kwahiyo tumekuja na mkakati kabambe wa kumwaga *Postinor-2* kwenye visima vyote vya kijiji ili mabinti zetu waweze kumaliza masomo yao salama.

Maparara: (*anashtuka*) *P-2*? Ile dawa ya...

Madalena: Hiyohiyo. Ya kuzuia ujauzito.

Maparara: Vipi kuhusu madhara ya dawa hiyo kwa wanaume wanaotumia maji ya visima hivi?

Madalena: Hicho ni kitendawili ambacho watakitegua wanaume wenyewe.

Maparara: Sio wazo baya. Napendekeza litafutwe pia suluhisho la upungufu wa nguvu za kiume ili mabinti wetu wasiikose haki yao ya msingi.

Madalena: Khaah! Tuzibatize maiti? Sote tunajua upungufu wa nguvu za kiume umesaidia kupunguza matukio ya ubakaji. Nafikiri tukiruhusu punyeto ya hadharani tatizo litakwisha kabisa. Mwanamke anakandamizwa sana. Na mimi siko tayari kukubaliana na hili. Fikiria, mwanaume anaweza

kutembea kifua wazi lakini mwanamke nguo fupi tu anasakamwa!

Maparara: Huoni kama ni jambo la heshima mwanamke kujisitiri?

Madalena: Ni woga wa wanaume! Mnajua wanawake wakitembea uchi wataiteka na kuitawala dunia!

Maparara: Ni rahisi kumuongopea anayekuamini.

Madalena: Uongo umejithibitisha kuwa taaluma inayolipa. Na watu wanaupenda. Ndio sababu tumeamua kuingiza kwenye mtaala wa Chuo Kikuu cha Nyinyoro ili vijana wetu wausome kama kozi. Ni matumaini yetu kuwa wahitimu wa kozi hii wataweza kujiajiri kwa urahisi. Hebu fikiria tuwe na maprofesa na madaktari wa Uongo! Fikiria kiwango cha maendeleo tutakachofikia!

Maparara: *(kwa hadhira)* Kozi ya Uongo chuo kikuu! Wale watu wafupi weusi wa kitongoji cha kule Magharibi ni wabishi na waongo sana kwa asili. Lakini kitongoji chao kina maendeleo gani? Mara mia ingeanzishwa kozi ya Uchawi tungetunza na kukuza utamaduni! *(mazungumzo yanaendelea kwa muda mrefu, hatimaye Maparara anaaga)*

Madalena: Kaka...

Maparara: Dada.

Madalena: Kinaitwa kuvuta zulia ulilokanyaga.

Maparara: Kitu gani?

Madalena: Unachofanya. Unafikiri unaijua dhambi? Bado unajifunza lugha hiyo. Ni mimi ndiye niliyekiandika Kitabu hicho. *(anamrushia kikopo cha mafuta)* Utauponza! *(wanatazamana kwa kitambo kidogo, Maparara anamwangalia Chegu ambaye ametulia tuli – macho na*

kinywa wazi akivuta pumzi fupifupi. Anatabasamu kwa huzuni, anatoka. Pazia linafunga)

Mandhari ya Pili

Nje ya Bucodiavolo. Ni usiku mchanga. Jengo lote liko kimya isipokuwa hatua za walinzi ambao wanazungukazunguka kuhakikisha usalama wa eneo hili. Taa ya chumba cha Madalena inawashwa, dirisha linafunguliwa. Vinatoka vitu kwa kasi na kudondoka karibu na Mlinzi-2 ambaye anashtuka na kuruka kando.

Mlinzi-2: Kitu gani hicho? Nimeona kama ni paka kamrukia kasuku! Na paka wa hapa alivyo na afya! Ha-ha-haa! Asilimia tisini ya Wanyinyoro hawamfikii.

Mlinzi-3: *(anafika)* Mkuu, nimeona vitu vikidondoka kutoka juu. Kuna usalama?

Mlinzi-2: *(ameduwaa. Mikononi ana viatu na kitabu cha Dkt. Dyaboli kiitwacho SEXUS: Siri za Ngono Tamu)* Viatu vya Kizibo.

Mlinzi-3: Nini? Viatu vya... Mungu wangu! Sikuwahi kufikiri siku moja nitakuja kuvigusa! Naweza?

Mlinzi-2: *(anampa. Yeye anafunua funua kitabu, anacheka kifala, anakiweka mfukoni)* Vitazame chap!

Mlinzi-3: Huyu amevijaza matambara ili vimtoshe na bado imeshindikana. Walitwambia Kizibo alikuwa na meno mabaya, hawakutwambia alikuwa na miguu mikubwa namna hii!

Mlinzi-2: Nguzo ya serikali ni siri kali.

Mlinzi-3: Halafu ni vizito! Kuvaa viatu hivi na kutembea mwendo aliotembea yeye ni jambo lisilowezezana karne hii. (*anavivaa. Vinampwaya*)

Mlinzi-2: Vilete hapa! Kwa miguu gani wewe uvae viatu hivi? (*anataka kuvijaribu pia, anasita*) Unaangalia nini sasa? Basi nitavijaribu nikifika nyumbani.

Mlinzi-3: Kizibo aliiishi misingi aliyoihubiri; lakini huyu, niamini, kama alikuwa hata na punje moja ya hekima aliyorithi, ameshaifuja yote pamoja na urithi wake mwingine. Niwie radhi Mkuu, nafahamu sipaswi kumzungumzia hivyo shangazi yako mbele yako.

Mlinzi-2: Afande, kuwa huru. Nafurahia kusikia ndugu zangu wakitukanwa.

Mlinzi-3: Fikiria, katika kijiji ambacho watu wanashindia mikate kama Wayahudi, na takribani asilimia tisini ya wanakijiji wanajifunika mashuka meusi ili kupunguza gharama za sabuni, unatumia mabilioni ya fedha kupima kiwango cha umaskini – tena kwa kuwauliza wanakijiji wanafanya mapenzi mara ngapi kwa wiki na chooni huwa wanatumia muda gani kumaliza kujisaidia!

Mlinzi-2: Walikumbuka kukuuliza kama una akili timamu?

Mlinzi-3: Kwanini waniulize hivyo?

Mlinzi-2: Inamaana hujui kuwa maskini ndio huwa wanatumia muda mrefu zaidi chooni?

Mlinzi-3: Mimi nipo hapa kwasababu tu nina familia inayonitegemea, na kupata kazi nyingine ni kazi.

Mlinzi-2: Maskini ni hanithi!

Mlinzi-3: Kwahiyo tuukubali uhanithi?

Mlinzi-2: Ukataeni. Ila ni mahanithi.

Mlinzi-3: Kwenye vijiji vya Kaanani ukitaka uonekane inabidi upige kelele!

Mlinzi-2: Bwa'mdogo; hapa ukicheka bila kuchekeshwa unaulizwa unamcheka nani, unapigwa. Ukipigwa usipolia unaambiwa una dharau, unapigwa tena. Ukilia unaambiwa unaleta uchuro, unapigwa ili unyamaze. Halafu ukinyamaza unaambiwa una kiburi, unapigwa tena. Ni mwendo wa kipigo tu! Na ukifa bila ruhusa ya Mkuu wa Kijiji familia yako inawajibishwa!

Mlinzi-3: Kwenye baadhi ya nyumba wapumbavu hustawi kuliko werevu.

Mlinzi-2: Unajua kwanini ni kosa la jinai kuamka alfajiri ukakimbia kwa kasi kuuzunguka mti ukiwa uchi?

Mlinzi-3: Kwani kinatokea nini?

Mlinzi-2: Unaona? Huna akili timamu wewe! Ukifanya hivyo unaweza kujilawiti!

Mlinzi-3: Shida hapa Nyinyoro wenye akili ndogo ndio wanawaongoza wenye akili kubwa. Kama huna ndugu mwenye jina ni ngumu kupata ajira.

Mlinzi-2: Unanitusi? Unamaanisha kwakuwa mimi nimeishia darasa la tano basi sikupaswa kuwa hapa na wewe kwakuwa umehitimu chuo kikuu ulipaswa kuwa sehemu bora zaidi? Chunga mdomo wako bwa'mdogo!

Mlinzi-3: Samahani Mkuu, sikumaanisha ku...

Mlinzi-2: Hapa hauhitaji makaratasi kijana; unahitaji watu! Ongea na mimi kwa adabu utafika mbali! Na elimu yako, unajua hata bahari ilipo? (*anakataa kwa kichwa*) Si unaona? Mbwa wewe! Na... (*mlio wa mlango ukifunguliwa*). Rudi kwenye lindo lako!

Mlinzi-3: Ndiyo Mkuu. (*anaondoka. Anafika Madalena, amevalia nguo ya kulalia*)

Mlinzi-2: Shangazi!

Madalena: Nimedondosha kitu kupitia dirishani. Nina uhakika unacho. Nakitaka.

Mlinzi-2: Ndio shangazi. (*anampa viatu*)

Madalena: Sio hicho. Kingine.

Mlinzi-2: Kingine?

Madalena: Nduku, ninapokuomba kitu, sio ombi! (*Mlinzi-2 anampa kitabu. Uso wa Madalena unaonesha tabasamu, anarejea ndani. Mlinzi-2 anavitazama tena viatu vya Kizibo, anatazama huku na huko, anavivaa. Ni vikubwa na vizito kiasi kwamba hawezi hata kuinua tu mguu. Haraka anavivua, anavitupa kwenye maua. Taa zinazima*)

Mandhari ya Tatu

Kichaka cha Miiba pembezoni kidogo mwa kijiji. Umbali wa takribani mita ishirini toka kwenye kichaka hiki lipo eneo jipya la makaburi ya kijiji. Limejengwa kwa bajeti kubwa: limezungushiwa wigo wa seng'enge madhubuti yenye ulinzi wa umeme na kutiwa geti la kifahari lenye picha ya peponi. Makaburi yamejengwa kwa mpangilio nadhifu na kutiwa nakshi na marumaru za bei ghali. Nyuma ya kichaka zinaskika sauti.

Maparara: Nimepata bahati nyingi hivi karibuni; lakini zote zilikuwa bahati mbaya. Nilibahatika kuonana na Madalena lakini niliumizwa na aliyoniambia.

Mwanakijiji-2: Alisemaje?

Maparara: Alisema ukiishi kwa mtu unakula kinachopikwa, sio unachotaka. Halafu akanipa mafuta akaniambia nitauponza.

Mwanakijiji-3: Utauponza mnini? (*hakuna anayemjibu*) Nipe mimi hayo mafuta. Mimi siogopi kuuponza!

Mwanakijiji-2: Ulimgusia kuhusu vilio vya Wanyinyoro juu ya ugumu wa maisha?

Maparara: Ndio. Akanikumbushia ile simulizi ya Mdomo Ulioponza Kichwa.

Mwanakijiji-7: Duh!

Maparara: Aligusia pia matamanio yake ya dunia mpya ya wanawake tupu bila mwanaume hata mmoja.

Mwanakijiji-6: Ningependa kuishi katika dunia hiyo.

Savo: Ukiwa mwanamke?

Mwanakijiji-6: Nikiwa mwanaume.

Savo: Wewe ni mpumbavu.

Mwanakijiji-6: Ningependa hiyo pia.

Mkyuba: Kingine alichosema?

Maparara: Alisema wanawake wote ni waongo.

Mwanakijiji-7: Basi usihofu kuhusu kuuponza.

Maparara: Kwanini?

Mwanakijiji-7: Alisema wanawake wote ni waongo.

Kwahiyo alipokwambia utauponza alikuongopea.

Maparara: Vipi kama aliposema wanawake wote ni waongo alikuwa pia ananiongopea?

Mwanakijiji-2: Tumuachie Mungu.

Mtoto wa Mganga: Mungu na Shetani ni marafiki; wanacheza drafti juu ya uso wa dunia na sisi ndio kete za mchezo – tunapoliwa wanatuweka kando, mchezo unaendelea.

Savo: Hak'yamungu unaenda jahanamu wewe!

Mtoto wa Mganga: Kwenye Kitabu Kitakatifu cha Nuru, Injili kama ilivyoandikwa na Gibu 3:7-9 inasema:

7 Jahanamu imehifadhiwa mahsusi kwaajili ya wale wanaoamini ipo. 8 Hata hivyo, habari za jahanamu zimetwa chumvi. 9 Moto kweli upo; lakini ni kwaajili ya kujipatia joto siku za baridi, kupikia chakula na kuchoma viapo vya wanasiasa.

Savo: Hiyo ni kufuru!

Mtoto wa Mganga: Kufuru ndiyo nini?

Mkyuba: Ni mwanadamu wa kustaajabisha. Madalena. Utotoni alikuwa anamuogopa sana baba'ke mzazi, na kila alipomuona alikuwa anamkimbia.

Mwanakijiji-6: Itakuwa baba'ke alikuwa mkali sana.

Mkyuba: Hapana. Ni kwasababu alikuwa mweusi sana.

Mwanakijiji-7: Ndiyo maana! Kumbe Madalena ni nazi!

Savo: Mimi nimeshachoshwa na mwenendo wa mambo ndani ya kijiji hiki! Kizibo alinionesha bahari ilipo; ajabu sikumbuki njia.

Mwanakijiji-2: U kijana mdogo sana kuanza kuchoka. Bado una takribani miaka thelathini ya kuishi. Miaka thelathini! Hiyo inamaanisha miezi mia tatu na sitini! Ni siku ngapi hizo? Ni masaa mangapi? Ni dakika ngapi? Unafikiri utautumia kufanya nini muda mwingi kiasi hicho? Umewahi kulifikiria hilo kijana wangu?

Mkyuba: Kumbe kuhubiri unaweza, mzee. Anzisha kanisa upige pesa!

Mtunza-makaburi: Jamani, tutahitaji kila mwanaume na mwanamke tutakayeweza kumpata ili kuongeza nguvu. Napendekeza kila mmoja wetu siku hiyo aje na mzazi wake mmoja.

Mkyuba: Naunga mkono!

Mwanakijiji-7: Mimi naomba nisijumuishwe kwenye pendekezo hilo kwasababu sina mzazi hata mmoja. Wote walishafariki.

Mwanakijiji-2: Kijana wangu, kupoteza mzazi mmoja ni kazi ya Mungu. Lakini kutokuwa na mzazi hata mmoja..., huo ni uzembe! Hakikisha kufikia siku hiyo uwe umepata walau mzazi mmoja.

Mwanakijiji-7: Lakini wazazi wangu wote... (*anasita anapoona wamemkazia macho*)

Mwanakijiji-6: Jamani, hamuoni kama kutekeleza tunachokipanga ni sawa na kuichoma moto nyumba yetu wenyewe? Kijiji hiki ni nyumbani kwetu. Kwanini...

Maparara: (*kwa ukali*) Nyumbani? Nyumba ni nyumbani kama wapendwa wako hawapo? Tazama kule. Lile pale ni eneo jipya la makaburi lililojengwa na serikali kwa hisani ya Watu wa Chaki na serikali imejitolea kugharamia shughuli zote za mazishi. Unajua hiyo inamaanisha nini? Tazama linavyovutia. Unaweza kulilinganisha na kule Mkanyageni unakoishi? Unaliona lile kaburi jipya lenye marumaru nyeusi na msalaba wa dhahabu? Lile ni kaburi la yule mjane aliyekufa kwa njaa nyumbani kwake halafu kwenye msiba watu wakala pilau-kuku na bia, na lile la kando yake ni la mwanawe aliyeuawa baada ya kuiba kitumbua kimoja gengeneni kwa mama Gubaguba. Lile pale lenye marumaru za kahawia ni la yule bwana aliyekufa kwa kipigo wakati akifanyiwa mahojiano kituo cha polisi. Lile refu lenye marumaru nyekundu na sanamu ya farasi ni la yule kijana aliyeimba wimbo wa Mbio, aliyeuawa kwa kukanyagwa na farasi wa Bucodiavolo siku ile alipoamrishwa ashindane nao mbio ili kuwaonesha wanakijiji kasi ya farasi! Yale saba yaliyopakana ni ya mke wa Bila na watoto wao wote waliouawa kwa kuchomwa moto usiku ndani ya nyumba yao. Bila mwenyewe tangu siku ile alipochukuliwa na Askari hatujui yuko wapi. Kizibo yuko wapi? Mkunga yuko wapi? Mwanakijiji-1 yuko wapi? Mahabusu na wafungwa magerezani wanavuliwa nguo zote kisha wanaamrishwa waruke kichurachura na kukohoa. Hii ni sawa kwako? Mmesikia kuhusu maiti kuokotwa zikiwa zimenyonywa damu. Unafikiri ni kitu gani kinawanyonya damu? Chegu si hayati si mamati; amekatwa ulimi na kila siku anadungwa sindano ya *Scopolamine*. Unajua *Scopolamine* inaufanya nini

ubongo wa mwanadamu? Unajua? Inakufanya unakuwa zombi! Unaweza kuwambia ndugu na marafiki wa watu hawa kuwa kijiji hiki ni nyumbani kwao? Niambie, watu wanapaswa kuogopa kabisa kusafiri baharini kwasababu meli moja ilikutana na dhoruba ikazama?

Mkyuba: Mambo ni segemnege. Kila kitu kimepanda bei isipokuwa pombe, sigara na kondom!

Mwanakijiji-7: Juzi nilikutana na bwana mmoja njiani. Tulipopishana tu akanishika shati akanivuta. ‘Kwanini unanipita bila kunisalimu? Unajua mimi ni nani?’ Nikaomba radhi nikamsalimu.

Mtoto wa Mganga: Njaa ndicho chakula kinacholiwa na wengi ndani ya kijiji hiki. Inaonekana mpaka kwenye kuta za nyumba.

Mwanakijiji-2: Mpaka mbwa wanabweka kama wana kikohozi. Njaa! Kuku na bata wamekonda na kunyonyoka kiasi kwamba si rahisi tena kutofautisha vishingo na wasio vishingo. Nyumba zilizokuwa na bustani za maua miaka ya nyuma, sasa zina bustani za mbogamboga. Majalalani mbwa na paka wanakula hadi viatu! Nani atupe ugali? Watu wanapokula samaki wanakula hadi mifupa, na inapotokea wakala nyama wanakaa na visu mezani.

Maparara: Unapotokea ubadhirifu wa milioni 50 inaundwa tume ya uchunguzi inayotumia milioni 500 kwenye uchunguzi!

Wengine: Hatujafa, lakini pia hatuishi. Yamkini kwa ufukara huu Mungu hatotaka kutuona jahanamu; ni dhahiri pia matajiri hawatatukaribisha peponi.

Mtunza-makaburi: Wanaume tunahofu mikopo tunayopewa ni mahari yetu; siku moja tutakuja kuolewa na Watu wa Chaki!

Mwanakijiji-6: Mnamlaumu kwa kutojitengenezea maadui nje ya kijiji?

Maparara: Ndiyo! Ikiwa anazo sifa nzuri za kustahili kuwa nao!

Mwanakijiji-6: Lakini pia kuna nguvu ya jina jamani! Zingatieni jina lake la asili.

Mwanakijiji-7: Kwani jina lake la asili ni lipi?

Maparara: Chindori! (*muziki wa mashaka unasikika*)

Savo: Tulichojifunza kupitia Kizibo ni kwamba kosa halipo kwa wengi wanaoshangilia upuuzi; lipo kwa wachache wanaouona na hawafanyi tofauti. Ndio sababu tulianzisha Nyota-ya-Moto. Isitoshe, kulipa kisasi kwaajili yako au kwaajili ya mpendwa wako sio tu ni haki bali ni wajibu! Aidha upo nasi au upo kinyume nasi!

Mwanakijiji-6: Tusifike huko ndugu zangu. Niwieni radhi kwa maneno yangu ya kipumbavu. Yameniponyoka tu, kama ambavyo kuna wakati maneno ya hekima hudondoka toka kwenye midomo ya wapumbavu. Nyinyi ni ndugu zangu.

Maparara: Apa.

Mwanakijiji-6: Jamani jamani! Mnajua...

Wote: APAA!

Mwanakijiji-6: Mimi Mwanakijiji-6, naapa kwamba nitabaki kuwa muaminifu kwa Nyota-ya-Moto na...

Maparara: Au acha tu! Kwanza viapo havina maana ndani ya kijiji hiki. Isitoshe...

Mtunza-makaburi: Shshshh! (*hatua za miguu zinakaribia. Wanachuchumaa, Mtunza-makaburi anakwenda kutazama. Anarejea na mtu*)

Fundi-majeneza: Ndugu zangu, mniwie radhi kwa kuchelewa. Nilipata dharura.

Maparara: Muhimu kuliko hii?

Fundi-majeneza: Msiba.

Maparara: (*kwa utulivu*) Ni nani awamu hii?

Fundi-majeneza: Yule msanii wa mvua inayowaka na jua linalonyesha. Yule aliyeimba ‘Prrrrrr! Wale, twaruka!’

Maparara: Imekuwaje?

Fundi-majeneza: Wametangaza amevunjika shingo akiwa anacheza mtindo wa ChiziKarogwaTena. Lakini chanzo cha ndani kinasema askari wamempandisha juu ya mlima wakamtupa chini ili waone kama alikuwa na uwezo wa kupaa. Jaribio la kisayansi lililoratibiwa na Watu wa Chaki.

Maparara: Tuwe tayari kwani hatujui nani atafuata.

Fundi-majeneza: Nafikiri tayari tunajua.

Wote: Kumaanisha...?

Fundi-majeneza: Mnakumbuka mwezi uliopita tulichukuliwa vipimo tukaambiwa serikali inataka kutushonea suti kama sehemu ya mkakati wake wa kuboresha muonekano wa kila Mnyinyoro?

Savo: Suti zimekuja?

Fundi-majeneza: Leo asubuhi nimeletewa oda ya kutengeneza majeneza tisa, na wakanisisitiza niyatengeneze kwa ustadi. Nilipouliza nini kimewasibu watu hawa nikaambiwa watapata ajali hivi karibuni.

Mkyuba: Unamaanisha walipata ajali hivi karibuni?

Fundi-majeneza: Watapata! Wengine watakufa kwa kichaa cha mbwa. Na nimeagizwa majeneza yote niyapake rangi za Bendera ya Kijiji. Ajabu ni kwamba vipimo nilivyopewa ni vile tulivyopimwa mwezi uliopita.

Maparara: Unavyo hapa?

Fundi-majeneza: Na futi nimekuja nayo ili kuhakiki kipimo kipi ni cha nani. (*anatoa mfukoni karatasi ya vipimo na futi. Anasoma*) 5'8 x 2'6-MMK. Nadhani hivi ni vipimo vyako. Hebu nikupime.

Mtunza-makaburi: (*anarudi nyuma*) Mh! Nini? Mimi siwezi kufa! Sitaki unipime!

Fundi-majeneza: Na wewe unakiogopa kifo?

Mtunza-makaburi: Ni vipimo vyangu kabisa! (*anakaa chini*) Sasa nani atalitunza kaburi langu?

Maparara: Hebu tusomee vipimo vingine.

Fundi-majeneza: (*anakohoa kidogo. Hofu imetanda, watu wanajifuta jasho*) 4'9 x 3'2-M6, 5'9 x 3'1-SVR,...

Mtoto wa Mganga: Ngoja! Vipimo vyote vina herufi mwishoni?

Fundi-majeneza: Vyote.

Mtoto wa Mganga: Nafikiri herufi hizo ni vifupisho vya majina. Hebu tusomee herufi tu za kila kipimo.

Fundi-majeneza: (*kwa msisitizo*) MMK.

Mtoto wa Mganga: Mtunza-makaburi

Fundi-majeneza: M6.

Mtoto wa Mganga: Mwanakijiji-6.

Fundi-majeneza: SVR.

Wote: Savonarola!

Fundi-majeneza: MPR.

Wote: Maparara!

Fundi-majeneza: MMG.

Wote: Mtoto wa Mganga!

Fundi-majeneza: MWT.

Wote: Mama Wanduta!

Fundi-majeneza: MKL.

Wote: *(kwa kusita)* Makelele?!

Fundi-majeneza: M2.

Wote: Mwanakijiji-2!

Maparara: *(kwa hadhira)* Hadi Makelele! Kweli baada ya mawindo mbwa hana thamani. *(kinasikika kicheko cha Kichaa)*

Savo: Hata hivyo ni bahati kubwa kuweza kuliona jeneza utakalozikiwa.

Fundi-majeneza: SIAMINI!

Wote: C-I-Mini? Huyu atakuwa nani?

Mtoto wa Mganga: Huamini nini ndugu yangu? Hebu tusomee jina la maiti nambari 9.

Fundi-majeneza: *(anajikakamua)* FMJ.

Wote: Fundi-majenezaaaaaa!

Mwanakijiji-3: Hilo ndilo lilikuwa la mwisho? *(Fundi-majeneza anakubali. Wote ambao hawakusikia majina yao wanapiga makofi wakishangilia)*

Maparara: Ndugu zangu, orodha hii inatuambia jambo moja: Hatuna cha kupoteza. Jeraha walilokusudia kututia tayari linavuja damu; nafsi wanazokusudia kuzitesa zishafikia kiwango cha mwisho cha mateso. Wengine mnaweza kudhani kwakuwa vipimo vya majeneza yenu havijafikishwa kwa

fundi basi mko salama, lakini niwaambie: hakuna aliye salama!

Mkyuba: (*anajipiga kofi kwenye makalio*) Hivi tunamzungumzia nani vile?

Mwanakijiji-6: Hata nikifa leo, nitakufa kwa furaha kwasababu katika siku nilizoishi nimefanikiwa kujifunza jambo kubwa ambalo hata wanazuoni hawalijui. Nimejifunza kwamba mwanamke anaweza kuwa na sura mbili na mioyo miwili.

Maparara: Hutokufa, mpaka utimize kusudi la kuumbwa kwako.

Mwanakijiji-6: Ni kusudi lipi hilo?

Maparara: Kupambana hadi utakapokufa!

Mwanakijiji-6: Basi nitamuumiza kwa hili. Sijajua kivipi bado, lakini nipeni muda. Siku itawadia atakuwa anaamini yu salama na mwenye furaha, halafu ghafla furaha yake itageuka huzuni na maumivu. Hapo, deni litakuwa limelipwa.

Maparara: Kuna towashi ndani ya Bucodiavolo tunaweza kumtumia. (*wanamtazama kwa shauku*) Unaweza kununua chochote ndani ya kijiji hiki. Isitoshe, wanasiasa ni makahaba tu – ukiimudu bei yao unaununua utu wao!

Savo: Kisa cha Yesu na Yuda. Siku zote kuna kahaba katika kila nyumba!

Maparara: Hivi mnajua kuna zaidi ya bilioni 800 zimefichwa hapo kwenye nyumba ya jirani?

Wote: (*wanatazama pande zote, wanaonekana kukanganyikiwa*) Lakini hakuna nyumba yoyote hapa jirani!

Maparara: Hakuna? Basi twendeni tukaijenge. Ageukaye ageuke jiwe! (*wanaondoka. Pazia linafunga*)

Mandhari ya Nne

Sauti ya kike toka nyuma ya jukwaa: Nilikuwa sijawahi kuchambua noti ya elfu kumi. Kumbe ukiichambua harufu yake inakuwa kama... *(mlio wa mlango ukifunguka. Pazia linapanda. Ni sebule ya Bucodiavolo. Wanawake wengi wamekaa wakichezacheza na Watu wa Chaki. Wapo pia Konde na Makelele wamejikunyata kwenye sofa ndogo wanatazama kwa uchu wakiwa wamebana miguu yao kwa nguvu. Ni sebule kubwa ya kifahari. Ukutani kuna picha ya Monalisa imeandikwa Ufunuo 23:27.*

Mtu wa Chaki-1: Kuheshimu muda ni tabia ambayo ni nadra kuikuta kwa mwanamke mrembo. *(Madalena anashuka ngazi za ghorofa, mkononi ana kitabu cha SEXUS: Siri za Ngono Tamu. Nyuma yake anakuja Kigego akiwa anarekebisha suruali yake)*

Madalena: Awamu ijayo kumbuka kutumia mkongo. Unakuwa imara.

Kigego: Waliniambia mninga ni imara zaidi. Nashangaa milango yote tayari imeliwa na mchwa.

Madalena: *(anawapa ishara wanawake waondoke sebuleni. Yeye na Kigego wanaketi)* Habari za mida jamani! *(Mtu wa Chaki-1 anarusha angani pesa nyingi za noti. Madalena, Kigego, Konde na Makelele wanainua nyuso zao kwa pamoja kuzitazama pesa hizo, halafu kwa pamoja wanainamisha vichwa vyao ambavyo vinaanza kutetemeka kwa nguvu kama wameingiwa na maruhani. Baada ya dakika*

kadhaa wanatulia, lakini macho yao yanaonesha hawako sawa, ndimi zao zinaning'inia na mate yanawachuruzika kwa wingi)

Mtu wa Chaki-2: Siasa ni kama ndoa. Na siku zote ninaamini mwanaume anayetaka kuoa anapaswa awe aidha anajua kila kitu au hajui chochote. Kigego, wewe ulikuwa unajua nini kwenye siku zako?

Kigego: *(baada ya kusita kidogo)* Nilikuwa sijui chochote, Mheshimiwa.

Mtu wa Chaki-2: Vizuri! Vizuri! Binafsi huwa sipendi chochote kinachotaribu kuuharibu ujinga. Maishani watu wengi hufanikiwa kwa kupitia ujinga; aidha wa watu wengine au wao wenyewe. Bahati nzuri mfumo wa elimu ndani ya kijiji hiki unalenga kuongeza ujinga. Kwahiyo ni rafiki wa utawala.

Konde: Elimu ya bure. Ha-ha-ha! Elimu gharama!

Mtu wa Chaki-3: Mnajua kwanini tulipendekeza nyumba hii iitwe Bucodiavolo? Mnajua maana yake?

Kigego + Madalena: Hapana.

Konde: Naamini maana ya jina haina maana.

Makelele: Ina maana. Sijui Bucodiavolo inamaanisha nini, lakini ni neno linaloskika vizuri masikioni. Mke wangu ni mjamzito; mwanangu ajaye nitamuita Bucodiavolo.

Mtu wa Chaki-4: Kizibo hakuwa mtu mbaya – hapana – lakini alikuwa mtu wa maudhi. Aliangukia kuwa mhanga wa misingi yake pofu ya kisiasa.

Makelele: Kizibo kilichofunguliwa kirahisi tu. Ha-ha-ha.

Mtu wa Chaki-1: Madalena, ushalifikiria lile suala?

Madalena: Umaskini ni ugonjwa wa akili. Dalili zake ni mtu kukosa kujiamini, chuki zisizo na msingi, kuwalaumu wengine na kujiua au kuwalazimisha watu wamuue. (*anatulia. Anafuta mate kwenye kidevu*) Nakubaliana nawe; njia rahisi ya kupunguza umaskini ni kuua idadi kubwa ya maskini.

Mtu wa Chaki-1: Kwa maendeleo ya sayansi, mwanakijiji anapojiua, ili kubaini kama alikuwa na ugonjwa wa akili au la, wanakijiji wengine kadhaa wanapaswa wawekwe katika hali kama iliyomfanya yule ajiue, ili kuona ikiwa wengi wao watajiua pia.

Madalena: Itafanyika hivyo, Mheshimiwa.

Mtu wa Chaki-6: Kizibo aliamini angeweza kuuua umaskini bila kuwaua maskini. Tulimcheka. Lakini ajabu alianza kufanikiwa. Yule bwana hakuwa wa kawaida! (*wanamtazama kwa hamaki*)

Kigego: (*anamtetea*) Aam, jamani, nafikiri Mheshimiwa hapa hakuwa na maana mbaya.

Mtu wa Chaki-1: (*anafungua begi lake na kutoa kitabu kikubwa chenye jalada jeusi lililoandikwa VIJILI VYA KAAANANI. Anakifunua*) Kijiji chako ni nambaaa...

Madalena: 912.

Mtu wa Chaki-1: (*anapokifikia anatabasamu. Anachukua kalamu na kukitia alama ya tiki*) Nyinyoro. Jina hili lina maana gani?

Kigego: Wengi hulitafsiri kama Malisho ya Kondoo, lakini kusema kweli, maana yake ni Shamba la Wanyama.

Mtu wa Chaki-5: Oh! Sasa naelewa kwanini Kizibo alitaka kulibadili. Alifunga ndoa na George Orwell.

Madalena: Mimi nafikiri tuliache hivyo hivyo.

Mtu wa Chaki-1: Mnazijua sheria na kanuni, sio?

Kigego + Konde + Makelele: Wimbo Mtakatifu wa Makanjanja!

Madalena: Wanyinyoro wamelala fofofo; ukiwatekenya, wanaota wanacheka – hawaamki, hadi uwafinye! Wanaona nacheka wanadhani nacheka nao; kumbe mimi nawacheka wao. Na hawa mbwa-koko wa Nyota-ya-Moto; walijaribu kuniua. Walilenga moyo ila wakaukosa. Mie sitowakosa!

Mtu wa Chaki-2: Waliukosa vipi moyo?

Kigego: Moyo wake uko upande wa kulia wa kifua chake; sio kushoto!

Makelele: *(anastaajabu) Dextrocardia!*

Mtu wa Chaki-5: Madalena, uko tofauti kabisa na yule bwana. Ajabu kati ya wote alikuchagua wewe! Hivi kwanini wanawake wazuri huzama hubani na wanaume wabaya, halikadhalika wanaume wazuri hudondokea mikononi mwa wanawake wabaya?

Kigego: Niliwahi kumsikia Kichaa akisema ni kani ya uvutano wa...

Konde: Alisema ni Usumaku wa Binadamu! Nakumbuka vizuri.

Kigego: Ndiyo, ndiyo. Usumaku wa binadamu. Ili kutengeneza urari wa mizani. Kama ambavyo pande mbili za sumaku zinazofanana hukwepana wakati zile zisizofanana huvutana. Alisema ili kuwe na urari ni lazima kuwe na pande mbili kinzani; joto na baridi, mchana na usiku, kike na kiume, Mungu na Shetani, kushoto na kulia, n.k. Kwamba mwanaume mkimya hawezi kudumu na mwanamke mkimya – nyumba itapoa na ndoa itaboa. Vivyo hivyo mwanaume

muongeeaji sana na mwanamke muongeeaji sana hawawezi kudumu – magomvi yatakuwa hayaishi. Ili uweze kutembea, ni lazima miguu yako ipishane; mmoja mbele mwingie nyuma. Vivyo hivyo, katika kupiga hatua, mguu wa kulia huenda sambamba na mkono wa kushoto; sio wa kulia. Ndivyo alivyoielezea.

Mtu wa Chaki-2: Unamuamini?

Kigego: Udadavuzi wake ulikuwa na mashiko. *(nje mvua kubwa inaanza kunyesha ikiambatana na radi, upepo na ngurumo za kutisha)*

Mtu wa Chaki-1: Simjui Kichaa huyu, lakini simpendi. Kichaa chake kinaambukiza!

Madalena: Hilo limeshashughulikiwa.

Mtu wa Chaki-1: Vema. Kwahiyo, hebu tudokeze; ile miradi ya maendeleo imefikia wapi?

Madalena: Zoezi la umwagaji wa P-2 kwenye visima vyote vya kijiji limeshafanyika. Mradi wa kutengeneza watu wa bandia kule Pigamiti unakwenda vizuri pia. Ni matarajio yetu kuwa ndani ya kipindi cha miaka kumi kila nyumba itakuwa na walau watu wawili wa bandia.

Mtu wa Chaki-2: Vizuri.

Madalena: Mgao wa umeme unaendelea kijiji kizima mpaka mzigo wenu uuzike uishe. Mpaka sasa yamesalia majenereta 219 na mitambo ya sola 192. Na tumeongeza kasi kwani sasa tunawawashia umeme kwa masaa manne tu kila siku.

Mtu wa Chaki-1: Mnawambia nini wanakijiji mpaka wanaendelea kuwa watulivu?

Kigego: Tunawakanganya tu, Mheshimiwa. Ninachokipenda kuhusu Wanyinyoro ni kwamba hata ukiwambia vinu vya kufua umeme vimepata *Menstrual Cramps* ndio sababu umeme umekuwa wa kusuasua, watahuzunika na kwenye ibada zao wataviombea vinu. Tukiona wameshikilia jambo hasi linaloihusu serikali, tunatengeneza tukio lingine la kulisimua katika jamii; mawazo yao yanahamia kwenye hilo tukio lingine.

Mtu wa Chaki-1: Watu wakarimu sana.

Makelele: Nakumbuka siku moja nilitamani kuona moto mkubwa, kwahiyo nikaamua kuichoma moto nyumba yangu. Kesho yake nikalalamika kwenye vyombo vya habari kwamba maadui zangu wa kisiasa walikusudia kuniangamiza pamoja na familia yangu. Wanakijiji wakaingia mitaani kuandamana wakilaani kitendo nilichofanyiwa. (*wote wanacheke sana*)

Mtu wa Chaki-7: Wajinga wanaishi ili kuwanufaisha wajanja.

Mtu wa Chaki-3: Na nyumba je?

Makelele: Ilikuwa na bima. (*wanacheke tena*)

Mtu wa Chaki-5: Twambieni kuhusu lile eneo la Mkanyageni tulilokubaliana mtupe kwaajili ya ujenzi wa kampuni ya kubeti.

Konde: Kule kuna changamoto kidogo. Wakazi wamegoma kuhama. Wanadai tulikowapeleka ni mbali na maeneo yao ya kazi.

Mtu wa Chaki-1: Kwahiyo...?

Kigego: Mvua inanyesha usiku huu. Nafikiri...

Madalena: Kunradhi. (*anaita*) Manunu! Manunu! (*kimya*)
We' mbwa!!

Mlinzi-3: Naam Mama! (*anaingia*)

Madalena: Yaani wewe mpaka utukanwe ndio unaitika!
Haya, mvua inanyesha umekaa tu; ili asubuhi usimwagilie maua? Chukua miavuli ukayakinge hayo maua yasinyeshewe, utayamwagilia asubuhi. Kazi ya mfanyakazi...

Mlinzi-3: ...ni kufanya kazi. (*anatoka*)

Kigego: Nilikuwa nasema huu ndio muda wetu wa kucheza. Tuvunje nyumba zao kwa tingatinga halafu asubuhi tutatangaza kwamba zilibomolewa na mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali.

Mtu wa Chaki-3: Tena umenikumbusha Kigego, nimekuletea zawadi toka Mjini; zidi kuboresha tabasamu lako. (*anampa mswaki*) Walikuita mjinga, lakini nakwambia; mjinga aliyefanikiwa kuzeeka sio mjinga!

Kigego: (*anajipangusa mate*) Ahsante Mheshimiwa. Halafu Mheshimiwa, kuna mwanakijiji meno yake yameanza kuwa meupe. Nitaomba unishauri jinsi ya kumfungulia kesi.

Madalena: Kigego na Makelele; Mkanyageni! Hakikisheni kila kitu kinakwenda sawa. Konde, wewe utakwenda na kikosi cha uokozi baada ya hawa kumaliza kazi yao. Mimi nitatuma waandishi wa habari na asubuhi nitafika eneo la tukio kuwapa pole wahanga.

Mtu wa Chaki-1: Vizuri! Ukimpora mtu, sema umefanya ili kumlinda asidhurike. Na ukimuua, kesho yake nenda uwasaidie ndugu zake kuchimba kaburi. Hiyo ndiyo siasa! Isitoshe, miradi yote hii ni kwaajili ya maendeleo ya kijiji

chenu. Ndugu Makelele hapa ni mmoja wa wasomi bora kabisa wa kijiji hiki na anaujua umuhimu wa miradi yote hii.

Makelele: Hakuna msomi kama mimi ndani ya kijiji hiki Mheshimiwa. *(Madalena anamkata jicho, ulimi nje)* Labda Madalena pekee!

Mtu wa Chaki-1: *(kwa Mtu wa Chaki-6)* Ambatana nao.

Mtu wa Chaki-6: *(anashika kilemba chake kichwani kisha anajishika uso na kukitazama kidole kinachotoka na unga wa chaki)* Lakini mvua inanyesha huko nje! Nita...

Mtu wa Chaki-2: Chukua koti la mvua! *(Kigego na Makelele wanashindana kuwahi chumbani kwa Mtu wa Chaki-6 kumletea koti. Makelele anasikika akipiga kelele ya hofu. Wanarejea Makelele akiwa na koti hilo mkononi. Kigego anatweta akishikilia kifua. Kwa pamoja wanamvalisha Mtu wa Chaki-6. Konde anawahi viatu vya mvua na kumvalisha pia kisha anapiga magoti na kuvipangusa kwa kitambaa chake cha jasho. Kigego, Makelele na Mtu wa Chaki-6 wanatoka)*

Konde: Lakini Madalena dada yangu, sidhani kama unapaswa kusoma kitabu hicho.

Madalena: Umewahi jiuliza kwanini waimbaji siku hizi hawaimbi tena kuhusu mapenzi bali wanaimba tu kuhusu ngono? *(anakataa kwa kichwa)*. Msomi mmoja aliwahi kuniambia maswali yote na majibu mengi ya maisha yanapatikana ndani ya kitabu hiki. Kaandae timu ya uokozi.

Konde: Sawa. *(wanatoka. Nje mvua inaendelea kunyesha. Inasikika sauti ikilalama kwamba panavuja chumbani; upande wa kichwa wa kitanda. Mbwa wanabweka kivivu. Bundi anasikika. Watoto wanalia. Wanawake wanapiga kelele*

kuomba msaada. Madalena anafungua dirisha la chumbani kwake anachungulia nje. Radi inamulika. Wanaonekana askari watano wakimshambulia kwa marungu Mwanakijiji-3 aliyetota kwa mvua. Mkyuba anapita akiwa anakimbizwa na mbwa watatu wa Askari. Anajikwaa anaanguka. Mbwa wanapomfikia wanasita. Wao wamenona kwelikweli; jinsi Mkyuba alivyokondeana, mfupa-na-ngozi, watamuuma wapi? Wanamuacha wanarudi walikotoka. Anainuka anaendelea kukimbia. Inasikika sauti ikifanya maombi):

Mhaya wetu uliye mbinguni,
Jina lako lipuuzwe,
Ufalme wako ufe,
Hapa duniani kama kuzimu,
Utupe leo ubabe wetu wa kila siku,
Usitusamehe makosa yetu,
kama tusivyowasamehe wanaotukosea.
Ututie majaribuni, na utuache maovuni.
Kwakuwa ubabe ni wako,
na nguvu, na utukutu, bata na misele.
Amina!

(Unasikika mlio wa bunduki. Madalena anashusha pumzi ndefu baada ya kuhitimisha sala yake)

Madalena: Watu wanapaswa kuelewa kwamba mbwa aliye hai ni bora kuliko simba aliyekufa. Isitoshe, mtu hawezi kuuawa mpaka awe anastahili kuuawa. *(anacheka. Unasikika wimbo:)* *Siamo Con Clavi, Siamo Con Dio, Siamo Con Il Nostro Dio Scuro. (anachukua kikombe kilichojaa damu ya binadamu, anainywa yote).* Damu ndiyo uhai. Acha moto uanze. Nguruwe, amani iwe nanyi. *(anafunga dirisha. Taa zinazima)*

Mandhari ya Tano

Mkanyageni. Ni moja ya maeneo maarufu wanayoishi watu wa hali ya chini kabisa. Nyumba zimebanana, ni fupifupi sana na nyingi zimejengwa kwa miti na mabati chakavu. Kwa kuziangalia harakaharaka, ukaongezea na harufu ya kifo iliyopo hapa, utasema ni mabanda ya nguruwe. Mvua inaendelea kunyesha. Makelele na Kigego wamefika hapa usiku huu. Tingatinga limeegeshwa karibu na nyumba ya Mama Wanduta, na Makelele ambaye ndiye dereva yumo ndani ya tingatinga pamoja na Mtu wa Chaki-6.

Makelele: Harufu ya hapa inachoma mpaka machoni! Mtu anawezaje kula au kupata usingizi katika eneo hili? Mchana nzi, usiku mbu. Hivi unajua maskini huwa wanavuja jasho mpaka ndotoni?

Mtu wa Chaki-6: Maisha ni picha isiyo na rangi; unachagua mwenyewe yako unaipaka rangi gani!

Makelele: Kweli. Ni kijiji huru. Halafu... unajua kama ni mimi ndiye niliyefanya ugunduzi kwamba jua lina jinsia ya kike, ndiyo sababu huwa linaogopa kutoka usiku. Na inaponyesha mvua usiku ni jua linakuwa limekosea kulenga kopo la kukojolea? Niliandika hii kwenye tasnifu yangu ya chuo kikuu.

Mtu wa Chaki-6: Kesho unaweza kugundua wewe ni kibwengo.

Makelele: Ugunduzi huo ndiyo ulionipa uprofesa!

Mtu wa Chaki-6: (anatabasamu kwa dharau) Hivi huyu ndugu yako ni chenjeu? Mbona amesimama tu hapo kama

mpumbavu! Au anadhani kwakuwa alinipa zawadi bahari na akampa Mtu wa Chaki-1 zawadi ya mgodi basi hiyo inamfanya awe spesho!

Makelele: Kige! Nangoja ishara yako tu!

Kigego: *(amesimama ananyeshewa mvua akiwa anakitazama kibao kilichoandikwa ‘usipOjiKAZA uNAKAZWA’ . Anajaribu kuking’oa, anashindwa. Anaiambia hadhira)* Wanamkumbuka. Bado wanaendelea kumwabudu. *(kwa hisia kali)* Kwenye siku zangu nilijitahidi sana, lakini walisema kitu pekee nilichokuwa nakiweza kilikuwa ni kuwaringishia meno yangu meupe – kwamba mbilikimo mie sikuwa naiona kesho ya Nyinyoro. Mama alipoamua nimuachie kiti ndugu yangu, yeye akanuia kuwaonesha wanakijiji bahari ilipo na jinsi ya kuifikia. Alikuwa kichaa, lakini walimpenda. Akaweka na sheria za uvunaji kwenye shamba la kijiji. Hapo ndipo vinyongo vilipoanza. Alipofikia maamuzi ya kuutema mate Wimbo Mtakatifu wa Makanjanja, nilijua alikuwa amevuka mstari. Kama Makelele, mimi pia sikushtushwa na taarifa za kutoweka kwake. *(anatulia. anatabasamu)* Kwahiyo naomba ieleweke vema: Sikuwa mlinzi wa ndugu yangu, pia sikuwa muuaji wake! *(anampa Makelele ishara)*

Makelele: Tunapaswa kuwasamehe maadui zetu; lakini baada ya kuwa tumewaua. Nilimuonya mwanamke huyu! *(anaendesha tingatinga linaivaa nyumba ya Mama Wanduta. Upande mmoja wa nyumba unabomoka. Wanduta na wadogo zake wanaskika ndani wakipiga kelele. Baba Wanduta anatokea mlango wa nyuma, tumbo wazi. Anashangaa kumuona Kigego. Kigego pia anashtuka; anafikiri upesi,*

anaanza kunengua. Baba Wanduta anaogopa baada ya kuona Kigego amepatwa na ugonjwa wa Kunengua. Haraka anarudi ndani. Kigego anampa ishara Makelele aharakishe.

Tingatinga linaimalizia nyumba na kusogea kwenye nyumba inayofuata, na nyingine, na nyingine, na kuendelea. Nyumba nyingi zilizokuwa zimesimama hapa sasa zimegeuka malundo ya miti na mabati chakavu juu ya ardhi. Chache sana zimesalia zimesimama. Tingatinga linaondoka. Baada ya muda vinasikika ving'ora vikikaribia. Serikali imetuma kikosi cha uokozi kuja haraka kuwasaidia wahanga wa ajali hii mbaya. Wanafika pia waandishi mashuhuri wa habari. Taa zinadimuadimua. Zinafifia. Zinazima.)

Mandhari ya Sita

Taa zinaanza kuwaka taratibu. Inaonekana Bucodiavolo. Ni ndani ya wigo wa kasri hili la kifahari. Ni usiku mnene kuelekea alfajiri. Mvua imekoma lakini bado kuna ngurumo na upepo kiasi. Anaonekana Kichaa akiwa anahojiwa na Mlinzi-3)

Mlinzi-3: Nakuuliza kwa mara ya mwisho. Umeingiaje humu na umekuja kufanya nini?

Kichaa: Nimefungua mlango, nikaingia. Usiku uliopita niliota joka limejizungusha linaula mkia wake lenyewe.

Mlinzi-3: *(kwa ukali)* Ndoto yako inanihusu nini?

Kichaa: *(anamtazama kifuni)* Una chuchu. Kwani unatoa maziwa?

Mlinzi-3: *(anajishika chuchu, anaziminya. Anasonya)* Kwani...

Kichaa: Unajua kwanini wenye akili ndogo ndio huwa wanakuwa na miili mikubwa?

Mlinzi-3: *(anajitazama)* Acha ufala! Mimi sio bongwe!

Kichaa: Sikia... Watu wanapaswa aidha kutomaswa au kuteswa. Ukiwasababishia madhara madogo watainuka kulipa kisasi; lakini ukiwatia ulemavu wa maisha hakuna watawachoweza kukufanya! *(Mlinzi-3 anamsukuma. Anapepesuka. Anageuka kwa kasi akiwa na mdenge wa baiskeli mkononi. Anamchoma kwenye shingo. Mlinzi anaanguka, anakufa. Muziki wa tanzia unasikika. Kilio cha*

mama ambaye wanawe wote wa kiume wamefanywa mashoga kinasikika. Ngoma zinaanza kusikika kwa mbali. Sauti ya ngoma inaongezeka hatimaye inaimeza anga. Mlinzi mwingine anakufa. Na mwingine, na mwingine, na mwingine. Kichaa anatoa ishara ya kusonga mbele. Nyota-ya-Moto wakiongozwa na Maparara wanapita kwa kunyata wakiwa na silaha mbalimbali. Mlinzi-2 anawanyatia lakini kabla hajawashambulia, nyuma yake anatokea Makelele na kumtia rungu la kichwa)

Mlinzi-2: *(akipepesuka) Kudadadeki! Maisha ni utani. Kumbe ni kweli dunia huwa inazunguka! (anakufa)*

Makelele: *Hongera! Umefanikiwa kulithibitisha hilo kabla hujafa (anamuonesha Maparara wapi wapite wakati yeye akiivutia kwenye maua maiti ya Mlinzi-2. Mtoto wa Mganga anakuja akiwa anaburuta nyundo kubwa. Kichaa anamuonesha akabomoe wapi. Anakwenda na kugonga kwa nguvu ukuta wa nyuma wa wigo wa Bucodiavolo; ukuta unabomoka. Inaonekana bahari! Anatabasamu. Anakwenda haraka ufukweni anakaa chini akiusikiliza ufukwe. Anacheka. Anageuka kuitazama hadhira. Anaanza kuongea kwa lugha ya Kichaa. Ngoja! Ana... Haiwezekani! Oh, maskini! Amekuwa kichaa! Ghafla Kichaa-1 anaganda kwa mshangao kwa kile anachokiona mbele yake. Nyota-ya-Moto wameambatana na Watu wa Chaki 7-12 ambao wamebeba silaha za moto. Tofauti na Watu wa Chaki 1-6 ambao wana vibiongo, pua zilizochongoka, na baadhi yao wanavaa kanzu na kufunga vilemba, Watu wa Chaki 7-12 wote wanaonekana wana usingizi. Mtu wa Chaki-7 ana kitabu chekundu, kama kile cha Mtu wa Chaki-1. Ghafla wanazungukwa na JWN na*

kuamrishwa wajisalimishe. Mtu wa Chaki-7 anarusha angani pesa nyingi za noti zilizo na rangi ya damu. JWN wanainua nyuso zao kwa pamoja kisha wanainamisha vichwa vyao ambavyo vinaanza kutetemeka kwa kasi. Baada ya dakika chache wanatulia. Macho yao sasa yamejaa damu. Wanaanza kupigana risasi wao kwa wao. Wanakufa wote! Kichaa-1 anacheka mpaka analia)

Kichaa-1: Utani gani huu! Walewale waliwao wa Liwale waliosema hawali wali wao wa Liwale. Siamini bado ningali mjinga! *(anafunua kidonda chake. Kimeongezeka ukubwa na sasa kinatoa funza. Muziki wa kishetani unasikika. Nyota-ya-Moto na Watu wa Chaki 7-12 wanafanikiwa kuingia ndani. Nyuma yao anafuatia Makelele. Anasita. Anaiambia hadhira)*

Makelele: Pengine mnaweza kuwa mnajiuliza imekuwaje nipo hapa leo. Kabla hamjanihukumu zaidi, sikilizeni hadithi yangu. Nimetoka familia duni sana. Wazee wangu walijinyima ili kuhakikisha ninasoma, nami nilijituma mpaka nikafanikiwa kufika chuo kikuu ambako pia nilihitimu kwa matokeo mazuri. Niliporejea mtaani baada ya kuhitimu, nikakutana na janga sugu la wazawa; *Uzoefu Angalu Miaka Mitatu!* Na kama mnavyoiua elimu ya Nyinyoro, hatufundishwi kujiajiri. Nilikaa mtaani mpaka nikawa naomba watu wafe ili nikale msibani. Nilitamani sana kukikimbia kijiji lakini sikujua bahari ilikokuwa. Siku moja nikakata shauri kwenda kumuona bwana mmoja aliyekuwa na mafanikio makubwa. Alicheka. Akaniambia vita vya mtaani hadi mawe yanahusika, kisha akanielekeza kwa mganga wa jadi waliyemuita Mkombozi. Kwanza nilisita, kwa kiwango cha elimu nilichonacho, niende kwa sangoma? Lakini yule bwana alinihimiza. Nikaenda. *(anacheka kwa dharau)* Elimu... eti ufunguo wa maisha.

Hivi unajua unajisikiaje unapobaini kwamba wewe ndiyo wa mwisho kugundua kuwa kitasa cha mlango kilishabadilishwa kwahiyo ufunguo ulionao hauwezi tena kukufungulia mlango? Kule niliwakuta wasomi na watu wengi mashuhuri, wote wakiwa kwenye foleni ya kumuona Mkombozi. Siku nilipoonana na Mkombozi, la haula! Unajua mshtuko niliokutana nao? Huyu Mkombozi nilikuwa namfahamu fika! Nilisoma naye darasa moja shule ya msingi na huyu ndiye alikuwa mbumbumbu wa shule. Walimu walitumia kila mbinu kumsaidia lakini ilishindikana, wakaamua kuwa wanamvusha hivyohivyo. Tulipofika darasa la nne aliacha shule na kuendelea kuchunga mbuzi wa babu yake. Halafu mimi baada ya kuwa nimehitimu Shahada ya Uzamivu chuo kikuu, eti leo nilikuwa hapa kumuomba anisaidie nifanikiwe. Ha-ha-ha! Basi, Mkombozi alinikumbuka; tukapiga soga nyingi hatimaye akanipa hiyo juju. Vilevile akanifunulia siri kwamba zipo njia mbili tu za kula na wakubwa kwenye vijiji vya Kaanani; kuwa mnafiki au kuwa na mikono michafu. Akasema kanuni ya asili ni kwamba simba anayemhurumia swala ndiye hufa kwa njaa. *(anatulia)* Nipo hapa leo; nina mafanikio makubwa. Pesa ni pesa; hakuna pesa inayonuka! Ha-ha-haa! Na... si mnajua mchimba-kaburi ndiye huingia kaburini kabla ya maiti? *(anaingia ndani. Vibwengo kadhaa vinatoka na kukimbia. Madalena anakurupuka chumbani alimolala na Watu wa Chaki 1-6. Yanaskika mabishano kwa sauti za juu. Madalena anatoka mbio akielekea baharini. Nyota-ya-Moto kadhaa wanamkimbiza. Watu wa Chaki 1-12 na wanawake wanawafuatilia. Madalena anaanguka ufukweni, anaomba msamaha akilia. Nyota-ya-Moto wanamzunguka, wanamtemea mate, wanamwambia atembee kama mbwa na abweke. Anafanya hivyo. Watu wa Chaki 1-12 na wanawake wanacheke sana. Nyota-ya-Moto*

wanaondoka na Madalena akiwa anaendelea kutembea kama mbwa na kubweka. Watu wa Chaki 1-12 wanaendelea kubishana na kutishana. Kichaa-1 anayaona haya kwa mbali. Ndani ya Bucodiavolo kuna mtu anasimama dirishani akimtazama. Anamlenga kwa bunduki, anamfyatulia risasi inayompata upande wa kulia wa kifua.

Kichaa-1: (anamtazama kwa mshangao. Anaongea kwa maumivu) Chora ramani yako mwenyewe, Minerva. Kamwe usitolewe ubaoni na watu wengine, hasa wanaume. Jua unachotaka, kifuate, pambana, ng'ang'ana! Ukijua jinsi ya kukipata, lala juu ya reli usiachwe na treni ya mwisho. Nilikuwa mjinga. Gabriella, nisamehe kipenzi changu. Nakupenda. (anapigwa risasi ya pili kwenye moyo. Anakwenda chini. Wakati huohuo Kichaa-2 anafika. Aliyefyatua risasi anarudi ndani upesi. Lakini Kichaa-2 amefanikiwa kumtambua. Ni Maparara.)

Kichaa-2: (kwa hadhira) Hivi kisasi ni sayansi au ni sanaa? Mimi ni mpambanaji. Ukimuua mbwa wangu, hakikisha unamficha paka wako. (analala kando ya mwili wa Kichaa-1 akitazama juu) Dunia ni msumari wa moto, na maisha ni shughuli ya mazishi isiyo na kikomo. Dunia imenipa nini? Mwanzo ni moto, mwisho ni majivu, na katikati ya mwanzo na mwisho ndipo yalipo maumivu yote ya maisha. Watu wanadhani amechukuliwa mtu, lakini si hivyo... kimechukuliwa kijiji! Kwanini msafisha-mazingira alisahau kusafisha macho yangu? Kila kitu ni kiza. Ee Mungu... Nakuomba uniangazie nuru ya mbalamwezi miguuni panguni ili nione kama kivuli changu bado kipo. (Jogoo anawika. Muazini anawakumbusha waja umuhimu wa swala. Anainuka. Anapiga mwayo. Anajikagua kama viungo vya mwili wake vyote vipo; anajishika kichwa, maskio, pua na mdomo kisha shingo, anajitazama kiwiliwili na mikono, anachungulia ndani ya suruali yake,

anatabasamu. Anajinyoosha. Anabeba furushi la Kichaa-1, anaondoka. Taa zinazima)

Kutoka gizani, zinaskika sauti kwa mwangwi:

Sauti-1: Naomba unisamehe mpenzi!

Sauti-2: *Musatanyoko!* Nilikuwa mjinga.

Sauti-1: Ningefanyaje Kizibo? Nyinyoro ina watu wachafu ambao hawanuki ila ukiwagusa unanuka wewe! Mie kwanza sikujua kama Bucodiavolo inamaanisha Tundu la Shetani. Na.. kusema kweli, sikuzaliwa mjamzito; yule mtoto ni wa Kigego. Mawazo yangu yalikuwa...

Sauti-2: Najua Madalena. Nilishapata tafsiri ya mawazo toka kwa Kichaa. Alisema mawazo ni mavitu ya kijingajinga ambayo wanadamu huyajaza vichwani mwao. Sasa namuamini kuliko wakati ule.

Sauti-1: Kwanini?

Sauti-2: Nilipokuwa hai nilikuwa nawaza kwamba kifo ni usingizi wa milele, kumbe kifo ndiyo mwisho wa usingizi. Maisha yote ni ndoto; kufa ndiyo kuamka toka kwenye ndoto hiyo ndefu. Kwakweli nimeelewa mengi baada ya kuja hapa. Nimeelewa hadi Ufunuo 23:27.

Sauti-1: Najua. Kwenye Biblia ya hapa Kitabu cha Ufunuo kinaishia 23:33. Ufunuo 23:27-33 inasema:

27 Na itajitimia kwamba baada ya neema ya karne sita, Mammon, mwana wa pekee wa Joka, atainuka kurejesha alichopoteza babaye. 28 Kulifanikisha hilo, Mwana wa Mfalme wa Kuzimu atajivika mwili wa mwanamke mrembo. 29 Lakini jicho la Bwana huona hata yaliyofichika. 30 Kutoka kwenye malango ya Mbingu, Bwana atamtuma Mwana-kondoo ambaye atafanya vita na Mammon. 31 Na atamuangusha. 32 Lakini si Mammon atakayeanguka – Tazama; itakuwa ni Mwana-kondoo. 33 Miili isiyo na nafsi itatembea duniani, usaliti utatamalaki, na...

Sauti-3: ...naapa kwamba, nitaiheshimu Katiba ya Nyinyoro, na nitahakikisha na... (*mbwa anabweka*)

Sauti-2: Hiyo sauti... Naijua sauti hiyo!

Sauti-1: Ipi? Ya mtu au hiyo ya mbwa-koko?

Sauti-2: Kwani ziko tofauti?

Sauti-1: Ni Maparara anaapishwa kuwa Mkuu wa Kijiji.

Sauti-4: Congratulations Mr. Maparara. We look forward to taking our bilateral ties to greater heights. Economic growth of Nyinyoro is our top priority. To begin with, we are offering you a loan of eighty thousand tonnes of stones for the construction of a higher wall to prevent the villagers from... (*wimbo wa maombolezo*)

“Parapanda italia, parapanda x2
Naye Madalena,
Atakuwa amekwishanyakuliwa,
Kwenda,
Kumlaki Bwan...”

Sauti-3: Thank you very much Mr. Ambassador. Though my father and mother forsake me, your face, Sir, I will seek. What are we without you? (*makofi, nderemo na vifijo*)

Sauti-4: With our newly-launched Time-travel Technology, we are going to help you travel back in time so you can rescue Kizibo before his death.

Sauti-2: Dah!

Sauti-5: Mkuu wa Kijiji hana nguo!

Sauti-6: (*nzito, ya kishetani*) Ha-ha-ha-ha-ha-haa!

MWISHO

VITABU VINGINE VYA MWANDISHI HUYU

ALMASI YA KIJANI: Magonjwa yote duniani yanatibika na kupona kabisa, lakini ulimwengu wa sayansi hautaki hili liwe wazi kwani magonjwa ni bishara inayowaingizia matrilioni ya dolari kila mwaka. Wenyewe wanasema *'huwezi kupata pesa nyingi toka kwa mgonjwa anayepona; mfanye aendeleo kuwa mgonjwa!'* Kitabu hiki kinakupa tiba mujarabu za majani, maua, mizizi na magome ya miti kwa magonjwa yote duniani!

TAFSIRI ZA NDOOTO: (kwa ushirikiano na Mchungaji Abel Muthembi, Sheikh Umar Al-Majid na Mganga wa jadi Snubi wa Mandembo) Huu ni Muongozo wa Jinsi ya Kuelewa Ndoto Unazoota Huwa Zinakwambia Nini ili uweze kuzitumia kwa manufaa na kuepuka mabalaa.

SEXUS: Siri za Ngono Tamu. Huu ni Muongozo wa Jinsi ya Kufanya Ngono kwa Usahihi ili kuridhishana na Kunufaika nayo, kihisia, kiakili na kiroho.

UJINGA WA BABA: Riwaya iliyosheheni siri na matukio ya kuisisimua.

MASHAIRI 101 TOKA GIZANI: Mkusanyiko wa Mashairi ya Ngono na Mapenzi.



+255 752 213 666



drdyabolimojo@gmail.com